Jumatatu Novemba 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581486

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com



**KANE AJIWEKEA REKODI BUNDESLIGA**

UKURASA 22

UKURASA WA 2

**Viongozi** wa dini walia na ubadhirifu alioanika CAG

UKURASA WA 17

**Mwinyi** kuzindua Taasisi Chuo cha Teknolojia India



UKURASA WA 19

SIKU 30 ZA GAZA:

**UN** yasema makazi na vituo vimejaa kupita kiasi

# Ajiua kwa sumu kisa mkewe kudai talaka

• **Yadaiwa** alikuwa anamsomesha chuo cha udaktari; Mtaalamu Saikolojia aonya wanaume... *Endelea ukurasa 2*



Abiria wanaosafiri kutoka mjini Muheza kwenda Tarafa ya Amani wakiwa wamekwama jana kutokana na Mto Msangazi kujaa maji kwa sababu ya mvua inayoendelea kunyesha. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## NEMC yasitisha uchimbaji dhahabu mtoni

UKURASA 16



## Mwalimu amwokoa mwanafunzi balaa la mapenzi ya jinsia moja

UKURASA 9

**MICHEZO** YANGA IPEWE MAUA YAKE KUIKANDA SIMBA 5G UK.24

**KATUNI** UK.6

# Adaiwa kujiua kwa sumu kisa mkewe kudai talaka

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KIJANA Nadhiri Kamala, Mkuu wa Idara ya Elimu na Wanafunzi Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA) Mkoa wa Mwanza, anadaiwa kujiua kwa kunywa sumu baada ya anayedaiwa mkewe, Yasinta (jina la pili tunalo) kumtaka ampe talaka.

Inadaiwa kuwa Yasinta alidai talaka kwa kuwa hakuwa tayari kuwa naye tena kimapenzi.

Kwa mujibu wa ujumbe wa mwisho wa kijana huyo katika moja ya kundi sogozi la mtandao wa jamii wa WhatsAPP la SMAUJATA usiku wa Jumanne Oktoba 31 mwaka huu, indaiwa kuwa mkewe huyo aliyemtaja kwa jina hilo la Yasinta, alimpeleka kusoma Chuo cha Udaktari Sumbawanga, lakini kabla ya mwezi kuisha alimtaka waachane.

"Jana tarehe 30/10/2023 alinitamkia kuwa kuanzia leo mimi siyo mume wake na anahitaji talaka yake bila kosa lolote na mimi siwezi kuishi bila yeye hapa duniani, hivyo ninautaarifu umma kuwa kweli wanafunzi wa vyuo hawaaminiki. Ngoja nimpishe aishi kwa amani," unasomeka ujumbe huo unaodaiwa wa marehemu Kamala.

Inadaiwa kuwa baada ya ujumbe huo, viongozi wa SMAUJATA Kanda ya Ziwa, wakiongozwa na Katibu wao, Hashim Ramadhani waliendelea na juhudi za kumfuatilia baada ya kuwa hapatikani katika simu yake ya mkononi.

Katika juhudi za kumfuatilia, walimkuta akiwa katika hali mbaya, akidaiwa kunywa sumu. Alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza (Sekou-Toure) ambako alilazwa kuanzia usiku huo wa kuamkia Novemba Mosi katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) hadi Novemba 4 alipofikwa na umauti.

Taarifa kwa umma iliyotolewa na Mwenyekiti wa SMAUJATA Mkoa wa Mwanza, Gasto Alex, ilithibitisha kutokea kwa kifo cha kijana Kamala kilichotokea saa sita mchana katika hospitali hiyo alikokuwa amelazwa tangu Oktoba 31 mwaka huu.

Ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa mwili wa marehemu ulikuwa katika Hospitali hiyo ya Rufani Mkoa wa Mwanza, huku wakishirikiana na familia kuandaa taratibu za mazishi.

Katika mazungumzo na Nipashe kuhusu kukithiri vitendo



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Azania wakiwa na wanachama wa Chama cha Wanawake Wahasibu, kwenye matembezi ya hisani kwa ajili ya kuchangia vitabu katika shule mbalimbali yakiwa ni maadhimisho ya Siku ya Uhasibu Duniani yaliyofanyika juzi, Dar es Salaam. HABARI UK. 4. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Viongozi wa dini walia na ubadhirifu alioanika CAG

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashehe ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini nchini, imesema ipo haja kuwawajibisha viongozi waliotajwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ubadhirifu wa fedha za umma.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Askofu William Mwamalanga alitoa rai hiyo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu kilichojiri bungeni wiki iliyopita.

Alisema viongozi wa dini wamekwenda mbali katika hilo, wamepanga kuandaa orodha ya majina ya mawaziri na maofisa waliotajwa kufanya ubadhirifu. Wataipeleka kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili viongozi hao wafutwe kazi mara moja.

"Hii ni aibu kwa taifa na wanamwaibisha Rais Samia ambaye amejitahidi sana kuomba mikopo ili kujenga nchi, lakini wachache wanafanya ubadhirifu," alisema.

Wiki iliyopita, bungeni kulikuwa na mjadala mkali wa ripoti za kamati za Bunge zinazoshughulikia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambazo ni Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Katika mjadala huo, wabunge walipendekeza adhabu kali kwa wabadhirifu ikiwamo kunyongwa huku wakitaka baadhi ya mawaziri wawajibike kwa kushindwa kuchukua hatua kwa watu waliotajwa kwenye ripoti ya CAG.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alilazimika kutoa ufafanuzi kuhusu wabunge waliojiandikisha wakitaka itungwe sheria ya kunyonga au kuwakata viungo wabadhirifu wa fedha za umma.

Alisema Bunge halijapitisha jambo lolote kuhusu kunyongwa wabadhirifu au kukatwa viungo na kwamba kwa sheria zilizopo sasa, Bunge litaendelea kusimamia serikali ili kuhakikisha wale ambao wanafanya ubadhirifu wanashughulikiwa.

# Sura ya bajeti ijayo ya serikali kujulikana leo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI leo itawasilisha bungeni mapendekezo ya Mpango wa Taifa na mwongozo wa kuandaa mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25 unaoanisha vipaumbele na mwenendo wa viashiria vya uchumi.

Katika uwasilishaji huo, Bunge litaelezwa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/24, mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Lengo la Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kuelekeza namna bora ya ukusanyaji mapato na utengaji rasilimali fedha za kutekeleza Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2024/25 ili kufikia mafanikio ya kijamii na kiuchumi.

Mwongozo huo pia unalenga kutoa maelekezo kwa maofisa masuuli wa wizara, idara zinazojitegemea, wakala wa serikali; sekretarieti za mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya umma kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na kisekta wakati wa maandalizi ya mipango na bajeti.

Vilevile, mwongozo huo utaonesha sera na mfumo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2024/25 ambayo inajumuisha mapitio ya mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi, mapitio ya utekelezaji mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24.

Pia mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25 ambao unaainisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/25 na muda wa kati pamoja na sera na mikakati ya kusimamia mapato na matumizi na uchambuzi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti, ukuaji wa uchumi na mikakati ya kukabiliana navyo.

Wiki iliyopita bungeni kulikuwa na mjadala mkali wa ripoti za kamati za Bunge zinazoshughulikia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambazo ni Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Katika mjadala huo, wabunge walipendekeza adhabu kali kwa wabadhirifu ikiwamo kunyongwa huku wakitaka baadhi ya mawaziri wawajibike kwa kushindwa kuchukua hatua kwa watu waliotajwa kwenye ripoti ya CAG.

Juzi, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, alilazimika kutoa ufafanuzi kuhusu wabunge waliojiandikisha wakitaka itungwe sheria ya kunyongwa au kuwakata viungo wabadhirifu wa fedha za umma.

Alisema Bunge halijapitisha jambo lolote kuhusu kunyongwa wabadhirifu au kukatwa viungo na kwamba kwa sheria zilizopo sasa, Bunge litaendelea kusimamia serikali ili kuhakikisha wale ambao wanafanya ubadhirifu wanashughulikiwa.

HABARI KITAIFA

# RC awahakikishia wananchi kupata maji

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge amewahakikishia wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuwa hali ya upatikanaji huduma ya maji ni nzuri kulinganisha na mwaka jana kutokana na mvua inayoendelea kunyesha msimu huu wa vuli.

Kunenge aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya kutembelea mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini kwa lengo la kukagua hali ya Mto Ruvu na uzalishaji katika mitambo hiyo kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

"Hali iliyopo kama mnavyojionea inaridhisha, ninapenda kupongeza watendaji wote wa Bonde la Wami Ruvu na DAWASA kwa ushirikiano mzuri na Ofisi za Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro kwa kuhakikisha changamoto iliyotokea mwaka jana ya upungufu wa maji haijajirudia.

"Kwa niaba ya wakuu wa mikoa wenzangu, niwahakikishie kwamba tunasimamia vizuri na jitihada zinaendelea kuhakikisha vyanzo vyetu vinaendelea na vinalindwa," alisema Kunenge.

Katika ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamidu Shaka ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, alisema ameridhishwa na hali ya Mto Ruvu na kutoa tahadhari kwa wanachi wanaoishi kwenye maeneo ya mabonde kuondoka mapema kwa kuwa mvua inaendelea kunyesha na inaweza kusababisha mafuriko.

"Tumejionea uhalisia wataalamu wametueleza kiwango cha maji kimeongezeka kwa asilimia 69, hili ni jambo kubwa na la kutia faraja, tuendelee na kuhimiza utunzaji wa mazingira.

"Tuendelee kuchukua tahadhari kama tunavyoshauriwa na vyombo vya hali ya hewa, ili kuepuka athari za mvua hii ikiwamo mafuriko," alisema Shaka.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji DAWASA, Shabani Mkwanywe alisema uzalishaji unaendelea kama kawaida, hivyo huduma ya maji ni ya uhakika.

Alitoa rai kwa wananchi kutoa taarifa kwa mamlaka endapo kutatokea uharibu wa miundombinu kipindi hiki cha mvua.

Itakumbukwa kuwa Novemba Mosi mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maagizo kwa wakuu wa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam pamoja na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dar es Salaam (DAWASA) kufanya ukaguzi na kuwaondoa wavamizi wote wa vyanzo vya maji, ili kuongeza upatikanaji wa uhakika wa maji katika mikoa hiyo.

Agizo hilo alilitoa wakati akifungua Mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia.

Alisema upungufu wa maji katika Mto Ruvu unachangiwa na ukame unaotokana na shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji kama vile ukataji miti kwa ajili ya kilimo na kuni, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa samaki katika mabwawa shughuli ambazo kwa kiasi fulani zimesababisha baadhi ya mito kukauka.




Mwongoza watalii wa Kampuni ya Utalii ya ZARA Tanzania Adventures, Gilbert Kasaba (kulia), akiwa na watalii kutoka Taasisi ya Tour Compass ya nchini Marekani katika kilele cha Mlima Kilimanjaro-Uhuru Peak mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

## Siku sita za Makonda Kanda ya Ziwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, anatarajiwa kufanya ziara ya siku sita mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Ziara hiyo ni sehemu ya kutekeleza ahadi yake aliyoitoa hivi karibuni katika mkutano wa kumkaribisha baada ya kuteuliwa na Halmashauri Kuu ya Chama hiyo, Oktoba 22.

Inatarajiwa kuanza Novemba 9 hadi 14 kwa kutembelea na kufanya mikutano ya hadhara katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu na Mara ambako atafanya mikutano ya kujitambulisha, kusikiliza kero na kuongea na wazee.

Makonda anatarajiwa kuieneza itikadi ya chama tawala, ikiwa ni baada ya miezi kadhaa kupita tangu chama kikuu cha upinzani nchini CHADEMA kupita katika mikoa hiyo ikieneza sera na maono yake.

Pia anatarajiwa kutembelea kaburi la Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli na akiwa mkoani Mara atatembelea kaburi la Rais wa Awamu ya Kwanza na Baba wa Taifa, Julius Nyerere, Butiama. Katika ziara hiyo, Makonda atabeba ujumbe wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya wanachama na viongozi wa chama hicho kama ilivyokuwa katika ziara yake mkoani Dodoma na itakuwa endelevu katika mikoa yote nchini.

Tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo Makonda amekuwa na utaratibu wa kutoa maelekezo kwa watendaji wa serikali kuhusu utatuzi wa kero za wananchi.

Kwa mujibu wa Makonda, maelezo hayo ni kutoka kwenye Chama kwa viongozi wa serikali kutimiza wajibu wao wa kuwahudumia wananchi na kuahidi kuwachukulia hatua watakaonekana kuangusha juhudi za chama na serikali.

Uteuzi wa Makonda unatazamiwa kuwa kichocheo cha kasi ya uenezaji wa itikadi ya chama hicho, ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya utendaji kazi kwa watumishi wa serikali wakiwamo mawaziri kutokana na kiongozi huyo kuahidi kutokuwa mwenezi wa watendaji wasiofanya vyema.

## Nchi 14 kushiriki tamasha la kusaka mbinu kukabili ukatili

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya watu 2,000 kutoka nchini na nchi zingine 13 duniani, wanatarajiwa kushiriki tamasha la 15 la jinsia lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa lengo la kubadilishana uzoefu na mbinu za kumaliza ukatili kwenye jamii.

Tamasha hilo litaanza kesho hadi Ijumaa katika viwanja vya TGNP, Mabibo mkoani Dar es Salaam, likifanyika sambamba na maadhimisho ya kitaifa ya miaka 30 ya mtandao huo na harakati za ukombozi wa wanawake.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, shirika hilo lililoleta chachu kubwa ya kuunganisha wadau mbalimbali kutoka vikundi vya wanawake, wanazuoni na mitandao ya wanawake kupata sauti ya pamoja katika ushiriki wa mkutano wa Beijing, mchakato ambao ulikuwa ni moja ya sababu kubwa ya kuanzishwa na kuimarishwa kwa asasi nyingi zinazotetea haki za wanawake nchini.

"TGNP ilianzishwa na imeendelea kutekeleza azma yake kuu ya kujenga harakati za nguvu za pamoja katika kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake ndani na nje ya nchi.

"Miongoni mwa njia zinazotumika kufikia azma hii ni kuanzishwa na kuendelezwa kwa majukwaa yanayowaleta wanaharakati kwa pamoja, moja ya majukwaa hayo ni Tamasha la Jinsia," alisema katika taarifa yake hiyo.

Alibainisha kuwa tamasha hilo linatambulisha mifumo iliyopo ya uchumi inayounga mkono mapambano ya wanawake na wanaharakati wa ukombozi wa wanawake wanaotaka ugawaji wa haki na usawa wa rasilimali, ikiwamo ya maji, bajeti za huduma za kijamii, rasilimali asilia kama ardhi, misitu na nafasi za uongozi na upatikanaji wa haki kwa watu wote.

"Msingi wa kila Tamasha la Jinsia hujengwa na tafakuri ya matamasha yaliyopita, likiongozwa na mada kuu na ndogo zinazotokana na tafakuri za dhana zinazohusu masuala ya kipaumbele ya wanawake na wasichana.

"Mijadala ya matamasha inatuwezesha kutambua kuwa mabadiliko haya yanaweza kufanikiwa, ikiwa wanawake watayaamini na kwa pamoja kuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa mambo yatakayotupa njia mbadala zilizo na mawazo ya kuleta usawa," alisema.

Mada zitakazojadiliwa kwenye tamasha hilo ni miaka 30 ya TGNP na Tapo la Ukombozi wa Wanawake, nyayo zetu, urithi wetu, simulizi za mabadiliko, changamoto na mikakati.

Alisema katika tamasha hilo mgeni maalum atakuwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UN Women duniani na Makamu wa Rais wa Afrika Kusini, akiwa ni mwanamke wa kwanza nchini humo kushika nafasi hiyo, Dk. Phumuzile Mlambo Ngcuka.

Mambo ya msingi kwenye tamasha hilo ni miaka 30 ya safari ya TGNP imetoa mambo ya kujifunza, uzoefu, uwekaji mikakati na mwelekeo ujao.

Lilian alisema tamasha la 15 linafanyika huku dunia ikiwa imezongwa na vikwazo hasa katika ugawaji sawa wa mapato na ukwasi wa dunia, vilivyopelekea kuwapo kwa ukwasi mwingi, maarifa na taarifa zenye mrengo wa wanawake na kwamba kuna haja ya kutoa msisitizo katika kuuondosha mfumo huo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 79/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU BORA ALLY CHAMBALA wa DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ASHA MOSHI SHABANI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 23 Mwezi 10 Mwaka 2023.

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC LAND APPLICATION NO. 196 OF 2023**

**TO: ALOYCE MAMKU**

**WHEREAS** the above named **APPLICANT** has instituted the **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in persons or by advocate or agent duly authorized on 8th day fo **NOVEMBER 2023** at **9:00 AM** before **Hon. K. MHINA J** in the mornig to answer the said **APPLICATION** and you are derected to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your replay.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on the day the said matter will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this court this 17th day of **OCTOBER, 2023.**

DEPUTY REGISTRAR

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 80/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOSHI SHABANI wa DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ASHA MOSHI SHABANI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 23 Mwezi 10 Mwaka 2023.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akimsikiliza Meneja wa Mkoa wa kihuduma DAWASA Kawe, Haruna Taratibu, kuhusu huduma zitolewazo na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) jana, alipotembelea banda la mamlaka hiyo, ili kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi wa Wilaya ya Kinondoni katika kongamano la wadau wa maendeleo ya mkoa lililofanyika viwanja vya Tanganyika Pakers Kawe. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wataalamu: Wananchi wajengewe uwezo zaidi biashara ya hewa ukaa

**Na Salome Kitomari**

WATAALAMU wa misitu kutoka nchi 10 waliokutana jijini Arusha hivi karibuni kujadili umuhimu wa ushirikishwaji kijamii na mifumo katika kugawana faida ya fedha za hewa ukaa Afrika, wamesema ni wakati mwafaka kwa wananchi kueleweshwa vyema namna biashara hiyo inavyofanyika.

Nchi hizo 10 zilieleza uzoefu wake katika kuwezesha biashara ya hewa ukaa na kwa kiasi gani wanaelimisha jamii, ili isiachwe nyuma katika kufanya biashara ya hewa ukaa kutokana na kutunza misitu kwenye maeneo yao.

Katika mjadala huo wa siku mbili ulioandaliwa na Jukwaa la Misitu Afrika (AFF) ulijikita kuangalia fedha za hewa ukaa, umuhimu wa ujumuishi na mbinu za kugawana manufaa.

Washiriki hao ni kutoka nchi za Congo, Tanzania, Uganda, Burkina Faso, Côte d'Ivoire, Ethiopia, Ghana, Kenya na Zambia. Uliandaliwa na Umoja wa Mataifa (UN) katika mpango wa kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na ukataji miti na uharibifu wa misitu.

"Tumekusanyika hapa kwa ajili ya kujengeana uwezo kama wataalamu ili tuwe na uelewa wa pamoja kuhusu REDD+, aina za fedha na vyanzo vyake kwa lengola kusaidia Afrika yetu kuwa na uelewa mifumo ya kimataifa na namna ya kuzipata fedha za biashara ya hewa ukaa kwa viwango tofauti," alisema Ofisa Programu Mwandamizi Prof. Marie- Louise Avana.

Alisema wataalamu wa nchi hizo pia wamejadiliana kuhusu uzoefu wa kila nchi walichojifunza tangu waanze kutekeleza, fursa zilizopo na changamoto ya kuzifikia fedha za kukabili mabadiliko ya tabianchi kutoka vyanzo mbalimbali.

"Tumekuwa na kujifunza kwa nchi na nchi, namna kila mwana jamii atakavyohusishwa kwenye hatua zote, muundo wa kunufaika unaofaa kwa nchi za Afrika," alisema.

Wataalamu hao wamekubaliana kuwa kuna kazi kubwa inafanywa na UN REDD na AFF katika kutoa nafasi ya kufanya mjadala na kujifunza kinachofanyika kimataifa hasa kwa nchi za Asia ambazo zimepiga hatua kwenye manufaa ya fedha za hewa ukaa.

Mengine ni kujua mbinu za masoko halisi na yasiyo halisi na changamoto ambazo nchi za Afrika zinapitia kunufaika na biashara hiyo na umuhimu wa kuhakikisha kila mwana jamii ameshirikishwa.

Aidha, wataalamu hao walisema kuwa nchi za Afrika zina hekta milioni 20.9 za misitu ikiwa ni asilimia 15.6 ya eneo lenye misitu duniani na kwamba hiyo ni hatua kubwa katika kufikia Agenda ya Afrika 2063 ya Afrika Tunayoitaka.

Watalaamu hao walisema misitu ni rasilimali muhimu kwa nchi za Afrika katika kutunza mazingira hasa katika kusaidia huduma za ikolojia kukabili uchafuzi wa mazingira, kuhifadhi udongo, upatikana na wa maji na hewa safi.

Pia walibaini kuwa katika kipindi cha mwaka 2008 hadi 2022 fedha za hewa ukaa zilizokwenda Latini Amerika ni asilimia 52 sawa na Dola za Marekani bilioni 1.5, kulinganishwa na Afrika asilimia 29 sawa na Dola za Marekani milioni 863 na Asia ni asilimia 11 sawa na Dola za Marekani milioni 616 huku asilimia nane ni kwa dunia na ukanda.

Katika mafunzo hao ilibainika kuwa nchi za Congo, Ghana, Ethiopia, Msumbiji na Uganda zimepiga hatua kubwa kwa kuwa na miradi mikubwa yenye fedha, ambayo kwa kiasi kikubwa imechangiwa na utashi wa kisiasa ulioruhusu kuwapo biashara ya hewa ukaa, mifumo thabiti na sheria ya kusimamia. Wataalamu hao pia walibaini kuwa nchi za Afrika zinapitia changamoto tofauti ikiwamo uelewa mdogo wa jamii, matarajio makubwa kwa wananchi wenye maeneo ya misitu, wanapata fedha haraka, utamaduni, imani na kukosekana sheria na kanuni za biashara hiyo.

# Kiini ongezeko la ajali chatajwa

**Na Halfani Chusi**

UKOSEFU wa elimu sahihi ya matumizi ya barabara kwa madereva kuhusu watembea kwa miguu kumetajwa kuwa sababu ya ongezeko la ajali kila uchao.

Sababu nyingine zilizotajwa ni ubovu wa miundombinu, kupuuza sheria, mwendo kasi na ulevi.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI), Maliki Barongo, alibainisha hayo kuelekea siku ya kimataifa ya semina ya usalama barabarani kwa wadau itakayoanza mwishoni mwa mwezi huu jijini Mwanza.

Alisema semina hiyo itakuwa mahususi kuangalia namna nchi zingne zilivyofanikiwa kudhibiti ajali, ili serikali iweze kutumia mbinu hizo.

"Tunaelekea kwenye tukio la semina ya kimataifa ya usalama barabarani itakayofanyika mwishoni mwa mwezi huu jijini Mwanza," alisema Barongo.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kubadilishana uzoefu kutoka kwenye nchi zilizoendelea namna walivyoweza kudhibiti ajali za barabarani mpaka kwenye ujenzi wa miundombinu.

Alipoulizwa kuhusu kilichowasukuma kuandaa semina hiyo, alisema wanalenga kuisaidia serikali kuongeza wigo wa uelewa kwa watumiaji wa barabara, ili kupunguza ajali ambazo kwa sasa limekuwa janga la kitaifa.

"Watu wanakufa, wanabaki tegemezi, ajali kila siku zinatokea, watu wanapata ulemavu wa kudumu. Ndio maana sisi tumeona kuna haja ya kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine kuandaa mafunzo hayo.

"Mwitiko ni mkubwa, watu wanapenda kujifunza na kupata ujuzi, serikali ijenge miundombinu bora zaidi hususani inayokidhi vigezo vya barabara kwa madereva na watembea kwa miguu," alishauri Barongo.

Aliwaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuunga mkono juhudi hizo akisisitiza kuwa baada ya mafunzo hayo watu watapata uelewa na hivyo ajali zitapungua kwa kiwango kikubwa.

# TAWCA kukuza taaluma ya uhasibu kwa kutoa vitabu vya wasioona

**Na Pilly Kigome**

CHAMA cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA), kimejipanga kuongeza wigo wa kukuza taaluma ya uhasibu kwa kutoa vitabu vya nukta nundu kwa ajili ya wanafunzi wasioona katika shule za sekondari na vyuo nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Hazina ndogo kutoka Wizara ya Fedha, Evance Asenga, alipozungumza na vyombo vya habari wakati wa matembezi ya hisani yaliyoandaliwa na chama hicho kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya taaluma kugawa katika shule za serikali.

Asenga alisema Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na TAWCA imejipanga kukuza na kuongeza idadi ya wahasibu wanawake nchini bila kusahau makundi maalum yanayoonekana kusahaulika kupata vitabu vya taaluma. "Changamoto bado zipo idadi ya wahasibu ni ndogo hasa katika taasisi za umma hasa mapato na matumizi na tunajitahidi kuongeza taaluma kwa bidii zote ili kufikia lengo," alisema Asenga.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu za Serikali, Prof. Sylvia Temu, alisema kuelekea Siku ya maadhimisho ya Uhasibu Duniani itakayofanyika Novemba 10, mwaka huu, bodi hiyo imekuja na matembezi hayo yanayolenga kutafuta michango ya kununua vitabu vya uhasibu na fani zinazoshabihiana na uhasibu kwa ajili ya kugawa shule za sekondari ili kukuza taaluma.

Alisema wanaamini kufanya hivyo kutachangia kwa kiasi kikubwa jitihada za kuboresha elimu ikiwamo na kuhamasisha wanafunzi wa kike kutorudi nyuma kubobea masomo hayo.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Wanawake Wahasibu Tanzania, Dk. Neema Kiure, alisema ununuzi wa vitabu hivyo ni kampeni maalum ya kuondoa dhana potofu kwa wanafunzi wa kike inayowaaminisha kuwa fani hiyo ni ngumu na ya wanaume pekee.

Alisema taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 2015 na wanachama 15 ikiwa na lengo la kuidhinisha wanawake wahasibu na kipindi hicho wakiwa asilimia 20 nchi nzima.

Kwa sasa nchini kuna wahasibu waliobobea zaidi ya 12,000 na wanawake ni asilimia 30 pekee.

"Tayari mwaka jana tulishagawa vitabu vya taaluma katika Shule ya Tuliani, Makurumla za jijini Dar es Salaam na Iyela ya mkoani Mbeya," alisema.

Mradi huo unalenga kuwaangalia mabinti waliokatiza masomo kwa kupata mimba za utotoni kuwafundisha ujasiriliamali na biashara ndogondogo na kuna wahitimu zaidi ya 260 katika miradi huo.

Mradi mwingine ni kuwafundisha elimu ya biashara kinamama wajasiriamali kutofautisha mitaji na matumizi binafsi.

## TANGAZO

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO KUANZIA TAREHE 6 NOVEMBA 2023

## Viwango unavyotozwa kadri unavyotumia (Na Kodi)

** - Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu
- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.09 kwa kila kilobaiti 10 za data

**VIWANGO VYA NDANI**

| Aina za simu | Bei (TSh/Dk) |
|---|---|
| Tigo - Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |
| Tigo - Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA - TIGO**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 720 | China, India, Marekani, Canada, USA, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi 3 | 1020 | Lebanon, Israeli, Hispania, Falme za Kiarabu, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi 4 | 1200 | Sweden, Hong Kong, Pakistani, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland, Pakistan, Yemen, Phillipines, Saudi Arabia, Netherlands, Japan, Malaysia, Norway, Ireland |
| Kundi 5 | 1800 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italia, Omani, Ujerumani |
| Kundi 6 | 2520 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 7 | 2520 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia |
| Kundi 8 | 19800 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA - ZANTEL**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 497 | Marekani, India, China, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Denmark, Sweden, Norway, Ireland, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani), Hispania, Ufaransa, Italia, Pakistani, Zimbabwe, Ujerumani |
| Kundi 3 | 1325 | DRC, Yemen, Omani, Lebanon, Israel, Sudani |
| Kundi 4 | 1500 | Zimbabwe (simu za kiganjani), Msumbiji, Malawi, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Mayote, Sudani ya Kusini |
| Kundi 5 | 1200 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 6 | 3000 | Cuba, Vanuatu, Tunisia, Tonga (simu za kiganjani), Tokelau, Uswisi, Somalia,Visiwa vya Shelisheli, Nauru, Samoa, Madagascar, Slovenia, Visiwa vya Comoro |
| Special | 18000 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA SMS**

| Aina za SMS | Bei (TSh/SMS) |
|---|---|
| SMS za kitaifa | 8 |
| SMS za kimataifa | 215 |

**VIWANGO VYA DATA**

| Intaneti | Bei (TSh) |
|---|---|
| Data kwa MB | 9.35 |

## VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

**MITANDAO YOTE**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 90 | 10 | 100 | 25 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 30 | 30 | 25 | 10 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 150 | 150 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1500 | 0 | 180 | 180 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 250 | 50 | 300 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 0 | 250 | 250 | 100 | 50 | Siku 7 |
| 3000 | 0 | 450 | 450 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 55 | 70 | 125 | 50 | 1024 | Siku 7 |
| 5000 | 100 | 180 | 280 | 100 | 1434 | Siku 7 |
| 5000 | 0 | 400 | 400 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 1200 | 1200 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 500 | 500 | 50 | 3072 | Siku 30 |
| 20000 | 0 | 800 | 800 | 50 | 7168 | Siku 30 |
| 30000 | 0 | 900 | 900 | 500 | 11264 | Siku 30 |

**SMS**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 200 | 0 | 0 | 0 | 200 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 0 | 0 | 1000 | 0 | Siku 7 |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 10000 | 0 | Siku 30 |

**BILA KIKOMO**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1000 | 0 | 30 | 30 | 50 | 0 | Bila Kikomo |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 250 | Bila Kikomo |

**INTANETI**

| Bei (TSh) | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 246 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 492 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 985 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 950 | Siku 7 | N/A |
| 2100 | 1024 | Siku 7 | N/A |
| 3000 | 1434 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 2458 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 4920 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 7373 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 4920 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 9830 | Siku 30 | N/A |
| 35000 | 17240 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 24576 | Siku 30 | N/A |

**KIMATAIFA - TIGO**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 40 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nigeria,Ghana - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Misri - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 4 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 80 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Nigeria,Ghana - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Misri - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 5 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 12 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Nigeria,Ghana - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Misri - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 180 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Ufaransa - Dk 13 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Nigeria, Ghana - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Misri - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 24 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Oman, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 38 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |

**KIMATAIFA - ZANTEL**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | China, India - Dk 22 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | Marekani, Canada - Dk 25 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Oman - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Pakistani, Hong Kong, Japan - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ufaransa - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Oman - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | China, India - Dk 110 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Marekani, Canada - Dk 110 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Pakistani, Hong Kong, Japan - Dk 25 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |

**HONORA TANZANIA PLC,**
PSSSF Commercial Complex, Kiwanja Na. 24, Kitalu Na. 3, Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P. 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

**www.tigo.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni mapato mlangoni inaua msisimko wa Dabi Simba, Yanga

**TARATIBU** ladha na msisimko mkubwa wa mechi ya watani wa jadi, 'Dabi (Derby) ya Kariakoo' kati ya Simba na Yanga, inaanza kushuka ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo majigambo kwenye vyombo vya habari yalikuwa yakitawala kutoka kwa klabu zote mbili hadi kuhamia kwa mashabiki ndani na nje ya nchi.

Derby ya Kariakoo imekuwa kivutio kikubwa si tu ndani ya nchi bali inavutia hata nje na hivi karibuni imekuwa ikitajwa kama moja kati ya 'dabi' kubwa na zenye mvuto mkubwa barani Afrika.

Aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga mwaka 2007, Mseribia Milutin Sredojevic 'Micho', ambaye analifahamu vema soka la Tanzania na Afrika kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kuiongoza timu hiyo kwenye Derby ya Kariakoo, huku akiwa na sifa ya kuwa kocha kwenye miongoni mwa Derby kubwa Afrika, hivi karibuni hukusita kuitaja mechi hiyo ya watani wa jadi ni moja kati ya Derby kubwa Afrika inayovutia.

Ikumbukwe Micho aliinoa Orlando Pirates ya Afrika Kusini kati ya mwaka 2017 hadi Agosti 2019, na nchini humo 'Soweto Derby' inayoikutanisha timu hiyo na Kaizer Chiefs, ndiyo mchezo wa watani wa jadi unaovuta hisia kubwa nchini humo na Afrika kwa ujumla. Lakini pia mwaka 2019, aliinoa Zamalek ya Misri, hivyo anaifahamu vema 'Cairo Derby', timu hiyo inapokutana na Al Ahly.

Kwa mantiki hiyo, Micho ni kocha mkubwa na mwenye uzoefu mkubwa wa Derby za Afrika, hivyo anaposema Derby ya Kariakoo ni yenye msisimko mkubwa na inayovutia zaidi Afrika, sisi ni nani hadi tumbishie mwalimu huyo anayelifamu vizuri soka la barani humu.

Hata hivyo, pamoja na Derby ya Kariakoo kukonga nyoyo za mashabiki, makocha na wadau wa soka ndani na nje ya nchi, sasa linaanza kupoteza msisimko wake kutokana na hamasa ambayo miaka yote imekuwa ikianzia kwa viongozi wote wa klabu, kuanza kushuka.

Katika hilo tayari Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imegundua kiini cha tatizo baada ya kueleza wazi kuwa inatokana na kanuni ya klabu mwenyeji kuvuna mapato yote ya mlangoni, hivyo klabu ngeni kuona hakuna haja kuupigia debe mchezo husika kwani utawanufaisha watani wao, hivyo kuliacha jukumu hilo kwa timu mwenyeji pekee.

Pamoja na Msemaji wa TPLB, Karim Boimanda, kueleza kwamba watalifanyia kazi kwa kukaa na viongozi wa klabu hizo kwani wanatambua mchezo huo si tu kwa ajili ya mapato bali ni mechi kubwa nchini na Afrika Mashabiki hivyo klabu zote mbili zinapaswa kupigia debe, sisi tunaona kuna lakufanya zaidi katika hilo ili hamasa kurejea.

Ikumbukwe sekta ya michezo kwa sasa ina nafasi kubwa katika kukuza utalii wa michezo nchini na Derby ya Kariakoo ni moja kati ya kioo cha soka la Tanzania kwa miaka yote na sasa inatajwa ni kubwa na bora zaidi barani Afrika, hivyo kuna haja ya kubadili kanuni hiyo ya mwenyeji kubeba mapato yote ya mlangoni kwa maslahi mapana ya mpira wa nchi hii.

Tunatambua kabla ya kuanza msimu mpya, klabu zote shiriki hutakiwa kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya kanuni na baadaye kuzipitisha kwa pamoja, hata hivyo mbali na mchezo huo wa Derby ya Kariakoo, pia Simba na Yanga huzinufaisha zaidi klabu za mikoani pindi zinapocheza ugenini, lakini kwa kuwa ziliridhia kanuni hiyo hilo hatupaswi kulitolea maoni kwa sasa.

Kubwa tunalotaka kuliona likifanyiwa marekebisho na TPLB kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), ni kuona haja kuanzia msimu ujao mechi ya Derby ya Kariakoo timu hizo zigawane mapato sawa katika michezo yote miwili ya ligi inayozikutana ili kurejesha hamasa na msisimko kuelekea mechi yao, hilo likiwa ni kwa masilahi mapana ya soka letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Wasanii Bongo achaneni na nyimbo zisizo na maadili

Na Adam Fungamwango

**WATOTO** wa Kitanzania wa kizazi hiki wanatia hata huruma, kwa sababu hawana nyimbo ambazo wanaweza kukaa, kuzisikiliza na kucheza kama ilivyokuwa zamani.

Wakiwa majumbani, mitaani, hata shuleni kwenye mahafali, sherehe mbalimbali na hata kupokea wageni wanaoleta misaada, wanahitaji nao wafurahi, wacheze, waimbe, lakini watafanya hivyo kwa nyimbo gani hizi za kisasa?

Nyingi zimekuwa na maneno yenye ukakasi, matusi na udhalilishaji kiasi kwamba hata unashangaa, mtunzi kweli alikaa chini na kufikiri kuwa hadhira anayoikusudia ina watu wazima tu, haitokuwa na watoto watakaokuwa wanaisikiliza na kuitazama?

Acha maneno, kwenye video ndiyo kabisa, kuna watu wanacheza nusu utupu, au aina ya uchezaji yenyewe nayo ni matatizo matupu mtu mwenye heshima zake kuangalia na familia yake au watu anaowaheshimu kama wakwe zake.

Juzi tu hapa kuna video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayoonesha wanafunzi wa shule ya msingi wakicheza wimbo wa 'Honey' wa msanii Zuchu.

Video hiyo iliyorekodiwa Tunduma ikamwibua Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, akaagiza walimu wakuu wa shule hizo wavuliwe vyeo.

Akizungumza Novemba 2, mwaka huu, nje ya Ukumi wa Bunge jijini Dodoma na Waandishi wa Habari, pia akapiga marufuku wanafunzi kucheza nyimbo zisizo na maadili na kuwataka walimu kuwa wasimamizi wa maadili pindi wanafunzi wawapo shuleni.

"Tumeshatambua shule yenyewe iko Tunduma, kulikuwa na kikundi kimeenda kutoa msaada shuleni pale, baada ya kutoa msaada ule kikaweka na muziki halafu wanafunzi wakacheza, na maudhui ya muziki wenyewe kila mtu ameusikia sina haja ya kuurudia.

"Tumeongea na wadhibiti ubora wapeleke taarifa kule, mkurugenzi awaondoe walimu wakuu wa shule mbili, moja shule ya Tunduma na nyingine ambazo ni kama shule pacha, waondolewe madaraka ya ukuu wa shule watafutwe wakuu wengine wa shule. Tunafanya hivi ili kutuma ujumbe, walimu wakuu tusaidieni msiruhusu vitu kama hivi viingie shuleni," alisema Profesa Mkenda. Wakati mjadala ukiendelea, BASATA nao wameibuka na kumfungia miezi sita msanii Whozu na faini ya Sh. milioni tatu kwa kuchapisha video ya wimbo 'Ameyatimba', una maudhui yanayokiuka kanuni za maadili kutokana na kuwapo ishara ya vitendo vinavyoashiria matusi.

Wasanii Mbosso na Billnas ambao wameshirikishwa kwenye wimbo huo, wao wamefungiwa kutojihusisha na muziki kwa miezi mitatu na faini ya Sh. milioni tatu.

Tunawapongeza BASATA, lakini kama wangekuwa makini sana, wangezifungia nyimbo nyingi mno. Yaani wasanii wengi wa sasa wanaona au kudhani wimbo ni lazima uimbe vineno vinavyoashiria matusi au kurekodi video zenye watu walio nusu utupu na uchezaji usio na staha.

Msanii ni kioo cha jamii, waige wanamuziki wa zamani walivyokuwa wakitunga nyimbo zao kwa maudhui mbalimbali kama, vita, kilimo, matatizo ya kijamii, matukio kama majanga, mafuriko, ajali, vifo, na waliimba hata mapenzi, lakini wao waliyaimba kifasihi zaidi na si kutaja maungo ya nguoni.

Ndiyo maana nyimbo za mapenzi za zamani baba anaweza kuimba hata na binti yake, hata mtu na mkwewe wala haina shida.

Hata wale wanafunzi wangeimba na kucheza wimbo kama 'Rangi ya Chungwa' au 'Georgina', sidhani kama ingeleta utata wa walimu kuvuliwa vyeo japo ni nyimbo za mapenzi.

Wasanii wa sasa wanatakiwa kubadilika kwani wanaweza kuimba wimbo usio na maneno ya ukakasi na ukapendwa kama ule wa Profesa Jay wa 'Baba' uliopendwa na kila mtu hata Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli.

Nadhani pia imefika wakati BASATA kuandaa semina na kufanya kampeni kubwa ya kuwataka wasanii waachane na kuimba aina hizo za nyimbo kiasi cha kuwafanya hata watoto kupata shida wanapotaka kufurahi na kucheza shuleni.

Kwa sababu hawana nyimbo zao, zote ni hizi hizi tu. BASATA inaweza ikakaa na kuandaa donge nono na tuzo ya mwaka kwa wasanii ambao wataimba au kutoa nyimbo za maudhui mengine kabisa na si mapenzi. Nadhani hapa sasa ndiyo tunaweza kuanza kuwafahamu wasanii wa kweli.

## HABARI KITAIFA

# Mabilioni yaongezwa miradi ya umeme

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI inatarajia kutumia Sh. bilioni 263.3 kutekeleza miradi ya umeme katika mikoa ya Iringa, Mara, Manyara, Mtwara, Rukwa, Ruvuma na Simiyu.

Ni baada ya kutia saini mikataba na makandarasi wa upelekaji umeme vijijini kupitia Mradi wa Ujazilizi fungu la pili C na B kwa upande wa fungu la pili C.

Kutiwa saini kwa mikataba hiyo ya nyongeza kumefanyika baada ya miradi mingine ya ujazilizi fungu la pili kutiwa saini Februari mwaka huu Ikulu jijini Dar es Salaam, ikihusisha mikoa ya Kigoma na Geita na kutekelezwa kwa Sh. bilioni 37.9 kwa ufadhili wa Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia shirika lake la maendeleo la AFD.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Hassan Saidy, akizungumza jana wakati utiaji saini mikataba hiyo, aliwataka makandarasi kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi na uadilifu ili kuondoa malalamiko ya wananchi dhidi ya serikali.

"Mwananchi anapokulalamikia wewe mkandarasi, ujue anailalamikia serikali, hivyo simamieni maadili na utendaji kazi sahihi wa wafanyakazi wenu vijijini," alisisitiza.

Alikemea vitendo cha baadhi ya wafanyakazi wa makandarasi hao kukata miti katika maeneo inakopita miradi hiyo bila kuwapa taarifa wananchi na kuonya kamwe havitakubalika.

"Japokuwa miradi ya umeme vijijini haina fidia, hiyo haiondoi haki ya mwananchi kwa kuwa eneo ni lake. Hivyo, tunatarajia kutakuwa na mawasiliano na uhusiano mzuri kati yenu ninyi makandarasi na wenye maeneo yao kabla hujakata mti, mfahamishe aelewe," alisema.

Saidy aliyataja mambo mengine yanayopaswa kuzingatiwa na kila mkandarasi wakati wa kutekeleza miradi hiyo kuwa ni pamoja na kutimiza lengo la serikali la kuboresha maisha ya wananchi kwa kuwafikishia umeme.

Alisema makandarasi wanaokwenda kufanya kazi vijijini wanapaswa kutambua kuwa ni waajiriwa wa serikali kulingana na mikataba waliyotia saini, hivyo wanapaswa kushirikiana na viongozi na wabunge kwa kuwa ni wawakilishi wa wananchi katika maeneo yao.

Pia aliwataka kuwajibika kwa viongozi hao kwa kuwapatia taarifa za maendeleo ya utekelezaji miradi hiyo, kuhakikisha wanawasimamia wafanyakazi wao wasijihusishe rushwa na kuepuka maneno yasiyo na staha kwa wananchi.

Alisema REA inafuatilia na kuhifadhi taarifa za utendaji kazi wa makandarasi hao, hivyo ikitokea yeyote kati yao akakataliwa kufanya kazi katika miradi itakayofuata ilhali utendaji kazi wake ulikuwa mzuri, ajue kuna sababu zilizomwondolea sifa, ukiwamo ukosefu wa maadili.

Alionya kuwa hakutakuwa na muda wa nyongeza wa utekelezaji wa miradi ambayo mikataba yake imetiwa saini.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa nchini, Celine Robert, ambao ni moja wa wafadhili wa miradi hiyo, alisema watafarijika kuona makandarasi wakitekeleza miradi hiyo kwa ufanisi.

Mkurugenzi wa Umeme Vijijini REA, Jones Olotu, aliwataka makandarasi hao kufanya kazi kwa mujibu wa mikataba waliyotia saini huku Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Mbadala na Jadidifu, Advera Mwijage akiwakumbusha kuwalipa vibarua wao kwa wakati na kuzingatia utunzaji mazingira.

Wakizungumza kwa niaba ya makandarasi wenzao, Baltazary Masindi wa Kampuni ya Sengerema Engineering Group Ltd na Aymen Louhaichi STEG International Services, waliahidi kutekeleza miradi hiyo kwa weledi, uaminifu, viwango na kukamilisha kwa wakati.




Wananchi wakipita kwenye maji yaliyojaa barabarani katika eneo la Makuti Temeke jijini Dar es Salaam kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Meno ya ndovu yawapeleka jela miaka 20

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi imewahukumu watu wanne, wakiwamo askari wawili wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani kila mmoja baada ya kukutwa na hatia ya kumiliki nyara za serikali bila ya kuwa na kibali.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Conslata Singano baada ya kuridhishwa pasi na shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Washtakiwa hao ni askari wa JWTZ namba MT 91209 Coplo Willson Peter Mkalala (32) na MT 90921 Coplo Oberd John Mwakatobe (34), Mikidadi Mohamedi Makalala (36) na Abdull Hemedi Kolela (32), wote wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Kabla ya kutolea hukumu, Hakimu Singano aliwapa nafasi ya kujitetea, kila mmoja kwa nyakati tofauti aliomba asipewe adhabu kubwa kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza, ana familia ya mke na watoto, pia wanategemewa na wazazi wao ambao ni wazee.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Singano alimwuliza Mwanasheria wa Serikali Godfrey Mramba kama ana kumbukumbu makosa ya zamani kwa washtakiwa na kudai kuwa hakuwa na kumbukumbu hizo huku akiomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwao na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

"Mheshimiwa Hakimu, makosa ya zamani kwa washtakiwa sina, hivyo ninaiomba mahakama yako tukufu kuwapa washtakiwa adhabu kali ikizingatiwa baadhi yao ni watumishi wanaotakiwa kulinda rasilimali za taifa letu," alidai Mramba.

Hakimu Singano, akitoa hukumu katika kesi hiyo Na. 06/2022, alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili. Sheria imemshika mikono, akawahukumu kila mmoja kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani kwa kosa la kukutwa na meno ya ndovu.


Mahakama hiyo pia iliamuru nyara hizo zilizokamatwa zikabidiwe kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kwa ajili ya utaratibu mwingine.

Pia gari aina ya Toyota Cruser T 873 BXY, mizani na simu walizokuwa wanatumia washtakiwa hao, zitaifishwe na kuwa mali za serikali.

Awali ilidaiwa mahakamani huko na Mwanasheria wa Serikali Mramba aliyesaidiwa na John Lema kuwa washtakiwa walikamatwa katika nyumba ya kulala wageni ya Nakivugo iliyoko Kata ya Nangando, Wilaya ya Liwale Novemba 14, 2021, wakiwa na meno mazima sita na vipande 30 vya meno ya ndovu yenye thamani ya Sh. milioni 371.

Mramba alidai kuwa kwa kuzingatia idadi hiyo ya meno, ina maana washtakiwa wameua tembo 15 na kuisababishia taifa hasara ya rasilimali zake.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Mikoa hatari uchomaji misitu yatajwa

Na Ashton Balaigwa,
MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)imeitaja mikoa minne ya Tanzania Bara kuwa hatari zaidi kwa uchomaji moto misitu na kusababisha uharibifu wa mazingira na kuchochea athari za mabadiliko ya tabianchi.

TAFORI katika utafiti wa moto unaoharibu misitu uliofanyika kwa kutumia satelaiti pia imeonesha eneo lililoungua katika mwaka 2021/22 ni kilometa za mraba 95,793 sawa na asilimia 9.8 kwa Tanzania Bara.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Revocatus Mushumbusi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipotoa taarifa fupi ya utendaji kazi wao katika masuala mbalimbali yakiwamo ya utafiti katika misitu na nyuki wakazi wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya ya kichama ya Morogoro Mjini.

Mkurugenzi huyo alisema utafiti huo unonesha mikoa ya Tabora, Lindi, Morogoro na Katavi iliongoza kwa matukio mengi ya moto misituni katika kipindi hicho.

Dk. Mushumbusi alitaja vyanzo vikuu vinavyochangia uharibifu wa misitu ni ufugaji, kilimo cha mashamba, uvunaji asali, majangili wanaoanzisha moto na moto mpango.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi hiyo wanaendelea kushirikiana na wadau kutoa elimu kwa jamii kuhusu vyanzo, athari za moto na mbinu za kukabiliana na moto katika maeneo ya hifadhi.

Dk. Mushumbusi pia alitaja utafiti mwingine uliofanywa unagusa afya ya misitu, umri wa kuvuna miti ya kigeni na utafiti wa kubaini vizazi bora vya miti.

Alisema taasisi inashiriki kuhamasisha wananchi kuanzisha mashamba ya miti ili kuimarisha ushiriki wao katika uhifadhi na kujipatia kipato.

Alisema taasisi hiyo imetengeneza teknolojia inayotumia simu ya mkononi kuainisha aina ya miti na maeneo ya kupanda (site species match tool - SSMT).

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini, Fikiri Juma, alitaka TAFORI kuongeza jitihada za utafiti ili kuja na matokeo yatakayosaidia kumaliza tatizo la uchomaji moto misitu kwa kuwa ni tegemeo kwa ustawi wa nchi wa vizazi vya sasa na vijavyo.




Mshindi wa promosheni ya Maokoto ndani ya kizibo ambaye ni mkazi wa Jet Lumo jijini Dar es Salaam, Rehema Rashid (kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. 500,000 kutoka kwa Mwakilishi wa Maendeleo ya Mauzo kutoka Serengeti Breweries Ltd Mkoa wa Dar es Salaam, Jemima Mtemi, katika hafla iliyofanyika baa ya Sunset jijini humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 900/- zadaiwa kutafunwa na madalali shamba la serikali

Na Julieth Mkireri,
KIBAHA

ZAIDI ya Sh. milioni 900, zinadaiwa kutafunwa na watu wanaodaiwa madalali na baadhi ya viongozi wa vitongoji wakati wa mauziano ya viwanja vya eneo la serikali la Mitamba (shamba namba 34) lililoko Kata ya Pangani, Halmashauri ya Mji Kibaha mkoani Pwani.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika mkutano na waandishi wa habari uliohusisha pia wakuu wa wilaya, wataalamu na wakurugenzi wa halmashauri, ukilenga kuelezea hatua iliyofikiwa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Alisema eneo la Mitamba, likiwa na shamba namba 34 lenye ukubwa wa hekta 4,000 lilivamiwa na wananchi na kuendeleza shughuli zao kinyume cha sheria.

Alibainisha kuwa hekta 2,963 kati ya 4,000 zilirejeshwa kwa Halmashauri ya Mji Kibaha kwa ajili ya kutumika kwenye shughuli za maendeleo na kubakiwa na eneo la hekta 1,037 ambazo hadi sasa zimebaki kwa Wizara ya Mifugo kwa ajili ya kufanya shughuli zake.

Licha ya kuwapo uhalali wa serikali kupitia Wizara ya Mifugo kumiliki eneo hilo, madalali waliendelea kuwauzia viwanja wananchi.

Hivi karibuni katika mkutano wake na wananchi wa Kata ya Pangani, Kunenge alitoa siku 14 kukamatwa viongozi 24 wakiwamo wenyeviti wa mitaa na watendaji walioshirikiana na madalali kuwauzia wananchi viwanja katika eneo la shamba namba 34 la Mitamba ambalo mali ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Kunenge alisema anayo orodha ya majina ya viongozi na madalali waliohusika kuwauzia kinyemela wananchi viwanja katika eneo hilo ambalo linamilikiwa na serikali na ataikabidhi kwa Jeshi la Polisi ili wachukuliwe hatua stahiki.

Mkuu wa Mkoa alisema tayari waliohusika na utapeli wa kuuza shamba namba 34 wameanza kuripoti kwenye vyombo vya ulinzi na usalama kwa ajili ya hatua za kisheria.

Pia alisema baadhi ya wananchi ni waoga kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kuwashughulikia madalali waliouza kinyemele ardhi inayomilikiwa na serikali.

Alisema migogoro mingi ya ardhi katika mkoa huo inasababishwa na wananchi kuvamia maeneo yanayomilikiwa kihalali. Mkoa unaendelea kuitatua kwa kufuata sheria.

Akizungumzia historia ya eneo hilo, Mpimaji Ardhi Halmashauri ya Mji Kibaha, Aron Shushu, alisema kiwanja hicho kilipimwa upya kwa kuzingatia Sheria Na. 8 ya Mipango Miji na kwamba mwaka 2021 kilifanyika kikao na wananchi hao kwa ajili ya kutoa katazo la kuvamia shamba hilo.

# 'Kujiamini ni nguzo muhimu wanavyuo'

Na Christina Haule, MOROGORO

KUJIAMINI kumetajwa ni nguzo muhimu inayopaswa kutumiwa na wanavyuo katika kutekeleza mambo mbalimbali kielimu.

Kaimu Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Dk. Elizaberth Mwakasangula, aliyasema hayo jana wakati wa warsha kuhusu ujuzi mtambuka iliyoandaliwa na chuo hicho kupitia Mradi wa Ufadhili wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi Kiuchumi (HEET).

Dk. Mwakasangula ambaye ni mratibu huo unaotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, alisema Mzumbe ni moja kati ya taasisi za elimu ya juu 14 zinazonufaika nao nchini nchini kwa sasa.

Alisema mradi wa HEET hushughulikia elimu katika maeneo saba ya mradi. Kati yake, asilimia 80 ya fedha zote za mradi ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu na wanatarajia kuwa na Kampasi ya Mzumbe nchini Marekani ambayo itakuwa ya kuvutia.

Alisema kampasi hiyo itatumika katika kujengea uwezo wanafunzi, kuweka huduma ya mitandao ambayo itasafiri hadi Kampasi Kuu Morogoro na kusaidia katika matumizi ya wanafunzi na kuboresha miundombinu ya Kampasi Kuu.

Dk. Mwakasangula alisema mradi wa HEET kwa kutumia kifungu cha tatu cha mradi wameweza kuwawezesha wahadhiri watano kufanya utafiti wa nje na kutoa elimu kwa ajili ya kukuza uchumi kwa kijamii.

Alisema wanavyuo wana wajibu mkubwa wa kufahamu zaidi juu ya ujuzi mtambuka sambamba na ujuzi wa kiufundi kwa kuweka mipango ya kujiamini zaidi kuliko ilivyo sasa.

Alisema upo msemo kwamba wengi wa wanafunzi si wa Kitanzania pekee bali pia dunia nzima, wanapomaliza masomo yao hawapati ajira kutokana na kukosa elimu ya ujuzi mtambuka.

Dk. Mwakasangula alisema ujuzi mtambuka ni namna mwanachuo anavyojionesha kimwonekano hasa katika mavazi, matendo na hata anavyojitambulisha.

"Serikali imeliona hilo, wapo wanafunzi wanapoambiwa kusimama kujitambulisha tu kwao ni shida, wanaanza kuinama chini hasa wa kike, lakini wakiambiwa kujieleza kwa kuandika wataandika hadi msomaji atachoka.

"Hili likifanyiwa kazi kwa upana litasaidia wanafunzi hawa kuinuka kielimu na nchi kwa ujumla," alisema.

Aliwaasa wanafunzi kutambua kwa kujifunza zaidi na kujua masuala ya ujuzi mtambuka kwa kujenga tabia ya kusikiliza wanayofundishwa, kusoma vitabu mbalimbali na kutumia mitandao ya kijamii kujifunza hasa suala la kujiamini.

Kaimu Amidi wa Shule ya Utawala na Menejimenti wa Chuo Kikuu Mzumbe, Idda Lyatonga, alisema warsha hiyo ni muhimu kwa kila mmoja wa wanafunzi itakayomsadia baada ya mafunzo hayo kuwa vizuri katika matumizi ya ujuzi mtambuka na namna ya kuutumika katika maisha yake yote.

Mmoja wa wanafunzi wa Mzumbe anayesomea masuala ya usimamizi wa afya (mwaka wa pili), Baraka Matiko alisema taaluma ya ujuzi mtambuka ni nzuri na inafaa kuingizwa kwenye mitaala ya elimu kwa wanavyuo. Inawasaidia wale wanaotaka kuwa wanasiasa au viongozi mahiri baadaye.

# Mwalimu apongezwa kumwokoa mwanafunzi mapenzi jinsia moja

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWALIMU Happyness Muro, mkazi wa Kibosho, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, amepewa 'kongole' na viongozi wa serikali za vijiji na wanaharakati, baada ya kufanikiwa kumwokoa mwanafunzi wa kidato cha tatu katika eneo hilo, aliyekuwa ameanza kushiriki mapenzi ya jinsia moja ya usagaji.

Mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), alikuwa akifanyiwa ukatili huo wa kingono na dada zake, ambao ni watoto wa mama mdogo.

Mwalimu Muro, alitoa ushuhuda huo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao kazi cha kuwajengea uwezo viongozi wa serikali ngazi ya vijiji, wanaonolewa na Shirika la kiraia la KWIECO, linalofadhiliwa wa Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), kupitia mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto.

Mwanafunzi huyo anayedaiwa kuanza usagaji akiwa darasa la tano, ni kati ya wanafunzi 20 waliookolewa na Mwalimu Muro, kwenye matukio ya ukatili wa kijinsia katika Kata ya Kibosho Magharibi. "Nimeokoa watoto wengi kwenye ukatili, mmoja ni mwanafunzi ambaye mama yake mzazi, alikuwa na watoto wengi wa kiume na huyo mmoja wa kike.

"Ili kumlinda mwanawe asiharibiwe, alimpeleka kulala kwa mama yake mdogo, ambako alikuwa analala na dada zake watoto wa mama mdogo. Wakati huo alikuwa darasa la tano; dada zake hao wakawa wanamfanyia usagaji (ukatili wa kingono).

"Sasa alipofika kidato cha pili, siku moja aliendа kutembea mtaani, akachelewa kurudi nyumbani, akajua akienda kwa mama mdogo kulala atachapwa.

...Ikabidi aende kwa bibi akalala, kesho yake akarudi kwa mama mdogo akaja shuleni. Mama akaja shule kuripoti na kudai huyo mtoto ameanza tabia sio nzuri na walimu wakaanza kumchapa."

"Wakati anachapwa, mimi natokea darasani nikakuta wanamchapa na kumhoji ili atoe majibu sahihi, nikawaambia mwacheni niwasaidie. Nilikaa na huyo mwanafunzi tukaongea kirafiki, nikamwambia utoe kwenye moyo wako wadhifa wangu kama mwalimu, tuongee mimi na wewe kama dada yako.

"Nikamuuliza ilikuwaje hebu nieleze, akaniambia mimi nililala kwa bibi ila nina kero yangu naomba usimwambie mama. Mimi nalala na dada zangu wa mama mdogo ila nataka niwakwepe kwa sababu wananisaga."

Baada ya kugundua shida ya mwanafunzi huyo, alirejea kuwaeleza walimu wenzake kwamba msichana huyo hakulala na rafiki wa kiume, isipokuwa alikimbia kitendo cha kusagwa.

Redempta Tarimo, amempongeza Muro kwa ujasiri wake na namna alivyoamua kumnasua na kubadili maisha ya mwanafunzi huyo.

Katika kikao kazi hicho kilichowashirikisha mabalozi wa nyumba 10 na wanaharakati kutoka vijiji vya Uchira, Karamsingi, Lole na Kibosho, mratibu wa mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto, Veronica Ollomi, alisema lengo la kikao hicho ni kujengeana uwezo wa kuimarisha jitihada za wananchi na viongozi wao, kutafuta suluhu ya matatizo ya ukatili wa kijinsia.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa nahodha Ali Hussen wakati akikagua boti ya mwendokasi ya abiria Zanzibar 3, baada ya kutia nanga juzi katika gati ya Bandari ya Tanga kwa mara ya kwanza ikitokea visiwa vya Unguja. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wanawake kujadili mustakabali kiuchumi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Anjela Kairuki, anatarajiwa kuongoza mamia ya wanawake wanaofanya kazi za utalii nchini, kujadili mustakabali wao kiuchumi, kupitia tamasha la wanawake festival litakalofanyika Novemba 17, jijini hapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa tamasha hilo, Nengasu Werema, alisema kuwa wameamua kuunga serikali mkono katika jitihada za kutangaza utalii.

Alisema wanawake watafanya tamasha hilo ambalo litashirikisha wadau wa utalii kwa pamoja ili waweze kushiriki kwenye sekta ya utalii.

"Tunataka kutangaza na kukuza sekta ya utalii kwa kuwa mada kubwa ya festival hii ni kuangalia namna ambavyo wanawake wanaweza kujihusisha katika sekta ya utalii ambayo itawezesha kukua kwa uchumi wa Tanzania na wa mtu mmoja mmoja," aliongeza.

Katika tamasha hilo kutakuwa na tuzo mbalimbali ambazo zitatolewa kwa wanawake vinara wa utalii, pia watatembelea vivutio vya utalii ikiwamo ya Hifadhi ya Taifa Ngorongoro na Hifadhi ya Tarangire.

Kamishna Msaidizi wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Jully Bede, aliwapongeza wanawake hao kwa kuandaa tamasha hilo na kuahidi kuwapa ushirikiano ikiwamo kuwaeleza wanawake fursa zilizopo kwenye hifadhi.

Mkurugenzi wa Wanawake na Utalii, Mercy Michael, alisema lengo la tamasha hilo ni kuwahamasisha kuunga mkono sekta ya utalii kuwekeza katika sekta hiyo na hatimaye kuongeza pato la taifa.

## Wanaoishi mabondeni Muheza watakiwa kuhama

**Na Steven William,** MUHEZA

SERIKALI imewataka wananchi waishio maeneo ya mabondeni katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, kuyahama makazi yao ili kuepuka athari mbaya za mvua ya El-Nino.

Agizo la kuwataka kufanya hivyo, limetolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala wilaya hiyo, Mohamed Mfaki, baada ya kuzuru makazi ya watu yaliyojengwa mabondeni na kwenye kingo za mito.

Mfaki, alishuhudia baadhi ya nyumba zikiwa zimejaa maji ndani na wakazi wake wakiwa wanaishi na maji hayo.

Alikutana na tatizo hilo katika Kata ya Genge, eneo la Kwamtiga, ambako alishuhudia pia Mto Amtiko, ukiwa umefurika na maji kuingia katika nyumba za watu na kuleta athari kubwa.

Wakati wa ziara hiyo, Mfaki, alikwenda katika makazi ya Abas Binijaji yaliyopo karibu na Mto Amtiko na kukuta imezingirwa na maji, na kuamuru wahame mara moja.

Katibu Tawala huyo, aliagiza wananchi wote ambao nyumba zao zipo mabondeni wahame haraka, huku akiwaagiza watendaji wa kata, watakaokaidi kuhama wakamatwe na kuwekwa mahabusu.

Vilevile, Katibu Tawala huyo, ametembelea kukagua ujenzi wa daraja jipya linojengwa katika Mto Amtiko eneo la Kwamtiga.

Alimtaka Mkandarasi wa Kampuni ya Mwalow Limited iliyopewa zabuni hiyo, Mbaraka Mwalongo, kuchukua tahadhari kipindi cha mvua kukamilisha ujenzi huo ili kuepusha ajali.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Muheza, Athanas Phares, alisema kuwa ujenzi wa daraja hilo utachukua miezi sita mpaka kukamilika kwake na mkandarasi yupo vizuri ameshafanya kazi maeneo mengi.





# Zaidi 12,000 wapata huduma maji Magu

**Na Vitus Audax,** MAGU

ZAIDI ya wananchi 12,500 katika Kata ya Chabula, Halmashauri ya Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza wameanza kupata huduma ya majisafi na salama kutoka katika Mradi wa Maji wa Bugando-Chabula uliotekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa zaidi ya Sh. bilioni 1.7.

Mradi huo umekamilika na kukaguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, mwishoni mwa wiki wakati akiendelea na ziara yake ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi mkoani humo pamoja na ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Akiwa katika mradi huo Makalla alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia serikali yake kwa kuhakikisha mradi huo unapata fedha na kukamilika kwa wakati ambako unaanza kuwanufaisha wananchi zaidi ya 12,500.

Alisema wananchi wanaonufaika na mradi huo ni kutoka katika vijiji vinne vya Bugando, Chabula, Nyashigwa na Kongolo, vilivyopo katika kata za Chagula na Kongolo wilayani hapa.

"Jukumu la wananchi sasa ni kuhakikisha mradi huu mnautunza ili utoe huduma endelevu na kuendelea kuwasaidia katika upatikanaji wa majisafi na salama, lindeni mradi huu uwapatie huduma hiyo muhimu ya kijamii kwa muda mrefu," alisema Makalla.

Vilevile, aliitaka jumuiya ya watumia maji kutoa ushirikiano wa kukarabati mambo madogo madogo ikiwa ni pamoja na kuumiliki mradi huo kwa kutokana na uhitaji wa upanuzi wa mradi huo na ongezeko la wananchi na wakati ukifika pawe salama.

Awali akielezea mradi huo, Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Magu, Mhandisi Daud Amlima, alisema kuwa mradi huo wa chanzo cha Ziwa Victoria, umefungwa pampu yenye uwezo wa kusukuma lita 75,000 kwa saa kwenda kwenye tangi la lita 250,000 na kwamba kuna vituo vya kuchotea maji 31.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chabula, Masatu Mgaya, aliishukuru serikali kwa mradi huo na kuiomba mamlaka husika kufikisha maji kwenye maeneo ambayo bado haujawafikia wananchi kwa kuwa awali walikuwa na shida kubwa ya maji kwenye vijiji hivyo.

Katika ziara yake endelevu, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alikagua ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Magu linalojengwa kwa awamu kwa zaidi ya Sh. bilioni 7.5 na kufikia hatua ya umaliziaji kwa asilimia 85 na alimwagiza mkandarasi kukamilisha mradi huo kwa wakati.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla (kulia), akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa kinamama katika Kata ya Chabula iliyopo wilayani Magu mkoani hapo, baada ya kukamilika kwa mradi wa maji wa Bugando-Chabula uliotekelezwa na RUWASA kwa Sh. bilioni 1.7. **PICHA:VITUS AUDAX**

# Mkandarasi aamuriwa kula sikukuu 'saiti'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amemwagiza mkandarasi kutoka Kampuni ya Elerai Construction anayetekeleza ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka mkoani humo, kutokutoka saiti kwaajili ya sikukuu za Krismasi kabla ya kukamilisha mradi huo.

Mndeme alitoa agizo hilo juzi alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi hiyo ambayo imefikia asilimia 60 na kumtaka mkandarasi huyo kukamilisha kwa wakati mradi huo.

Alisema ofisi hiyo ni muhimu kwa wananchi kupata huduma ya msaada wa kisheria na kudai haki zao na kuagiza kufikia Desemba 29, jengo hilo liwe tayari limekabidhiwa na Januari 2, 2024, Mkurugenzi wa Mashtaka aanze kufanya kazi akiwa ndani ya ofisi hiyo mpya.

"Mkandarasi umeaminiwa fanya kazi, pesa zipo na hakuna kisingizio cha kuchelewesha ujenzi wa ofisi hii, fanya kazi hadi siku ya Sikukuu ya Krismasi, tunaka ianze kufanya kazi mwakani, huduma za kisheria ni muhimu sana kwa jamii," alisema Mndeme.

Mkandarasi kutoka kampuni hiyo, Mhandisi Hussein Msuya, alimwahidi Mkuu wa Mkoa kwamba ujenzi huo watakamilisha kwa wakati, kwa sasa wapo kwenye hatua za umaliziaji.

Alisema ujenzi wa ofisi hiyo waliuanza mwaka jana na hadi kufikia Desemba mwaka huu watakuwa wamekamilisha na kuikabidhi, ujenzi huo unagharimu Sh. bilioni 2.1.

## Kata tano Msalala zapata vituo vya afya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATA tano za Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, zimepata vituo vya afya na kusogeza huduma za matibabu karibu na wananchi hali iliyodhibiti adha ya wajawazito kutembea umbali mrefu kufuata huduma hizo katika hospitali za wilaya.

Kata hizo ni pamoja na Isaka, Segese, Bulige, Mwalugulu na Mwanase ambako wananchi walilazimika kufuata huduma muhimu katika Hospitali za Wilaya hususani pale wanapokosa huduma katika zahanati zilizopo katika maeneo yao.

Hayo yamebainishwa na Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddi Kassimu, katika kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 kilichoenda sambamba na uzinduzi wa jengo la ofisi la halmashauri hiyo, uliogharimu Sh. bilioni 4.3.

Kassimu alisema, kituo cha afya Isaka kimekamilika na sasa kinatoa huduma za matibabu kwa wananchi na vijiji na kata za jirani, awali walilazimika kusafiri umbali wa kilometa 30 hadi 40 kwenda katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kupata matibabu.

Vile vile, wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za usafiri wa Sh. 3,000 hadi 5,000 hususani wajawazito walilazimika kujifungulia nyumbani na kuhatarisha usalama wao pamoja na vichanga vyao tumboni, lakini kwa sasa huduma zimesogezwa karibu na hakuna tena malalamiko ya wananchi.

"Vituo vya afya vya Mwalugulu, Segese, Bulige na Mwanase, viko hatua ya mwisho ya ukamilishaji ili vianze kutoa huduma kwa wananchi na ifikapo mwishoni mwa mwezi Desemba 2023 vitakuwa vimekamilika pamoja na baadhi ya majengo ya hospitali ya wilaya iliyojengwa Kata ya Ntobo," alisema Iddi.

Hata hivyo, alisema mwaka wa fedha uliopita wa 2022/2023 halmashauri ilipokea Sh. milioni 750 kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika vituo vya afya hivyo na hospitali ya wilaya na vitakapokamilika kwa muda uliopangwa watahakikisha wanapeleka vifaa tiba ili kuanza kutoa huduma mapema.

Diwani wa Kata ya Mwalugulu, Flora Sagasaga, alisema ujenzi wa kituo cha afya Mwalugulu unaoendelea umefikia asilimia 95 na unatarajia kukamilika hivi karibuni na kuiomba Wizara ya Afya utakapokamilika wafikishe vifaa tiba na dawa na kuanza kutoa huduma kwa kuwa wanaoumia ni wanawake, watoto na wazee.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Hamisi Katimba, alisema vituo vya afya Segese na Bulige viko hatua ya mwisho ya ukamilishaji na ifikapo mwezi Desemba, mwaka huu, vitakuwa vimekamilika, kwa sasa baadhi ya huduma ya mama, baba na mtoto na wagonjwa wa nje (OPD) zimeanza kutolewa.

Pia alisema, wamejenga jengo la kisasa la ofisi ya halmashauri kwa thamani ya Sh. bilioni 4.4 kati ya hizo Sh. bilioni 4.3 zimetumika.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema awali miradi mikubwa ya kimkakati ilikuwa ikisimama na kushindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha, kutokana na kupangiwa bajeti kwa mfano ya Shilingi bilioni tano, lakini inayofika na kuanza ujenzi ni Shilingi bilioni mbili.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI SABA BORA WA UEFA WA WAKATI WOTE UK. 12-13



BELLINGHAM

# WACHEZAJI WANNE WAPYA WANAOFANYA VIZURI ULAYA

**LONDON,** England

USAJILI wa mchezaji mpya daima unachukuliwa kuwa mojawapo ya uimarishaji bora wa kikosi ambao klabu inaweza kufanya. Kadhalika, ni fursa nzuri kwa klabu kufanya uwekezaji mpya kwa mustakabali wake.

Wakati wa dirisha lililopita la uhamisho wa majira ya joto barani Ulaya, mikataba kadhaa na ubadilishaji wa wachezaji ulifanyika huku klabu nyingi zikijaribu kurekebisha kasoro katika vikosi vyao.

Ingawa hayo hapo juu yamekuwa ya manufaa kwa baadhi ya klabu hadi sasa, makala haya yanaangalia wachezaji wanne wapya wanaofanya vizuri zaidi Ulaya hivi sasa...

**#4 James Maddison (Tottenham Hotspur)**

Kuna msemo kwamba wachezaji bora wanaweza kubadilisha utendaji wa jumla wa kikosi. Kweli, imethibitishwa kwa mara nyingine kwani James Maddison amebadilisha si safu ya kiungo tu bali pia safu ya ushambuliaji ya Spurs hadi sasa.

Mwingereza huyo ameweza kutumia vema ubunifu wake wa kushambulia, kwani ametengeneza nafasi nyingi kwenye Ligi Kuu England (25) msimu huu na anashika nafasi ya pili.

Pia amesajili michango saba ya mabao katika michezo tisa ya timu yake na hii imeongeza matokeo ya timu msimu huu.

**#3 Harry Kane (Bayern Munich)**

Mchezaji wa kiwango cha juu ambaye angepata njia ya kuzoea kila wakati anaweza kutumiwa kuelezea vema ni Harry Kane, kwani amekuwa bora mbele ya lango tangu ajiunge na Bayern Munich.

Kane amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Bundesliga, kufunga mabao 12 katika mechi tisa za mwanzo tangu ajiunge na Bayern Munich na amesajili pasi za mabao tano. Namba zilizo hapo juu zinazungumza zenyewe, kwani pia zinaonesha darasa wazi. Kwa hiyo, bila shaka ni mmoja wa washambuliaji wazuri zaidi barani Ulaya, mshambuliaji huyo wa Kiingereza bado amethibitisha kuwa mmaliziaji mzuri. Kane, hata hivyo, anatarajiwa kushinda kombe kuu huko Bayern Munich msimu huu.

**#2 Victor Boniface (Bayer Leverkusen)**

Mnigeria huyo bila shaka ni miongoni mwa dili bora zaidi katika dirisha la usajili lililopita, kwani amekuwa akipiga mipira yote mbele ya lango msimu huu. Boniface amekuwa mzuri kumtazama katika safu ya ushambuliaji msimu huu, kwani amekuwa mzuri katika mashindano yote ambayo ameshiriki hadi sasa.

Kwa upande wa namba muhimu za ushambuliaji, Boniface amefunga mabao tisa na kusajili 'asisti' tatu katika mechi 10. Hata hivyo, mbali na namba zake za ushambuliaji, uwapo wake umesaidia kukuza mbinu za Xabi Alonso kwani uwezo wake wa kuwavutia mabeki umekuwa muhimu katika kutengeneza nafasi kwa washambuliaji wengine kuimarika. Kwa hivyo, anapaswa kupongezwa kwa michango yake hadi sasa.

**#1 Jude Bellingham (Real Madrid)**

Walio bora zaidi kati ya wengine wanaweza kuonekana kama matamshi muhimu kuonyesha jinsi Jude Bellingham amekuwa wa kipekee na muhimu kwa Real Madrid tangu ajiunge na klabu hiyo

Kiungo huyo wa kipekee wa England amekua kutoka kufunga mabao ya kuamua mechi hadi kuwa mfungaji bora wa klabu katika msimu huu. Mchezaji huyo amekuwa kwenye orodha ya mabao mara 13 katika michezo yake 13 ya kwanza akiwa mchezaji wa Real Madrid. Pia, amesajili asisti tatu katika michezo hiyo. Namba zake zinajieleza zenyewe, kwani kwa sasa hakuna mchezaji mpya aliyesajiliwa Ulaya ambaye amefanya vizuri zaidi yake hadi sasa.


## ISIKUPITE

HAT-TRICK aliyoipiga Harry Kane juzi dhidi ya Borussia Dortmund, inamfanya kufikisha mabao 15 akiwa na Bayern Munich msimu huu na hiyo ndiyo idadi kubwa zaidi ya mabao kwa mchezaji yeyote kwenye historia ya Bundesliga katika mechi 10 za kwanza. Hiyo inamaanisha pia sasa amefunga mabao 20 kwa msimu huu huku 10 kati ya hayo akifunga katika mechi zake tano za mwisho kwa klabu na nchi yake. Hat-trick hiyo pia ni ya pili mfululizo kwake kwani wiki moja iliyopita alifunga nyingine wakati Bayern Munich ikiisambaratisha Darmstadt kwa mabao 8-0.



## Extra Time

# WACHEZAJI SABA BORA WA UEFA WA WAKATI WOTE


RONALDO

**NYON,** Ufaransa

LIGI ya Mabingwa Ulaya (UEFA), ambayo mara nyingi hujulikana kama kilele cha soka la Klabu za Ulaya, ni mashindano ambayo yanakamata ndoto na matarajio ya kila mwanasoka. Yanasimama kama hatua ya mwisho ambapo klabu hutoa wachezaji wa kiwango cha juu zaidi duniani.

**Kufanya vema katika Ligi ya Mabingwa ni tamanio kubwa kwa wachezaji kwani inawapa nafasi ya kuandika majina yao katika historia ya soka.**

Nguvu isiyo na kifani ya shindano hilo, nderemo na vifijo vya mashabiki wanaojaza viwanja vya kihistoria na fursa ya kujinasua dhidi ya mastaa wa zao hilo vinaifanya kuwa hatua ya kuvutia tofauti na nyingine.

Wachezaji bora pekee katika historia ndio waliofaulu katika mashindano haya adhimu na wameweza kuacha alama isiyofutika kwa ujuzi wao, matukio ya kukumbukwa na mkusanyiko wa mataji yanayotamaniwa.

Hapa tunawaangalia wachezaji saba bora zaidi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa wakati wote, haya sasa...

### #7 Paolo Maldini

Paolo Maldini anasimama kama mmoja wa wachezaji bora katika historia ya hadithi ya UEFA. Akitumia taaluma yake yote ya miaka 25 pale AC Milan, Maldini alikuwa kielelezo cha uthabiti na ubora kama mlinzi.

Gwiji huyo wa Italia alicheza jukumu muhimu katika mafanikio ya Milan mwishoni mwa miaka ya 1980 na 2000, akishinda mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Pia alimaliza kama mshindi wa pili katika misimu mitatu pamoja na kushinda Ligi ya Europa mara mbili kabla ya shindano hilo kubadilishwa kuwa Ligi ya Mabingwa.

Umahiri wake wa kipekee katika ulinzi, utulivu kwenye mpira na uongozi uwanjani ulimfanya kuwa gwiji wa kweli katika mashindano hayo.

### #6 Xavi Hernandez

Xavi Hernandez anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi katika historia ya UEFA kutokana na usanii wake wa ajabu wa safu ya kiungo na mafanikio yake makubwa akiwa na Barcelona.

Uwezo wake wa kudhibiti kasi ya mechi na uchezaji wa kupiga pasi za uhakika ulimfanya kuwa mcheza safu ya kati wa kiwango kisicho na kifani.

Xavi alikuwa muhimu katika enzi kuu ya Barcelona, ambapo walishinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa, akionesha maono yake ya ajabu na akili ya soka kwa utaratibu mkubwa.

Uthabiti wake na utulivu chini ya shinikizo katika mechi za Ligi ya Mabingwa vilikuwa muhimu katika ushindi wa Barcelona.

### #5 Karim Benzema

Karim Benzema amekuwa mmoja wa wachezaji wenye ushawishi mkubwa wa Real Madrid katika karne ya 21. Shukrani kwa ustadi wake mzuri na sifa za kipekee za kiufundi, Benzema alifanikiwa kuvinjari mabadiliko mengi ya nafasi na kukabiliana na mbinu za makocha kadhaa wakuu.

Benzema ameshinda jumla ya mataji matano ya Ligi ya Mabingwa akiwa na Real Madrid, lakini ni ushindi wao wa msimu wa 2022-23 ambao ulimpamba sana. Mfaransa huyo alitoa matokeo mengi ya ushindi wa mechi haswa katika hatua ya mtoano na kuwapaisha Real Madrid katika kinyang'anyiro hicho.

### #4 Andres Iniesta

Mshirika kipenzi wa Xavi wa kiungo Andres Iniesta pia ni mmoja wa wachezaji wakubwa katika historia ya UEFA. Uwezo wake wa kuchezea mpira na kuzunguka kwenye nafasi zinazobana, ulimfanya kuwa tishio mara kwa mara kwenye safu ya kiungo na kumwezesha kutengeneza nafasi nyingi za mabao kwa timu yake.

Maono ya ajabu ya Iniesta na utulivu chini ya shinikizo vilikuwa muhimu katika ushindi wa mara nyingi wa Barcelona wa Ligi ya Mabingwa wakati akiwa na klabu hiyo.

Mchango wa Iniesta kwenye Ligi ya Mabingwa, ambapo mara kwa mara alionesha maonyesho ya kiwango cha juu, inaimarisha urithi wake kama mmoja wa wababe wa muda wote wa shindano hilo. Alishinda jumla ya mataji manne ya Ligi ya Mabingwa katika maisha yake ya kifahari.

### #3 Luka Modric

Luka Modric anachukuliwa kama mmoja wa viungo bora wa karne ya 21. Michango yake imekuwa muhimu kwa utawala wa Real Madrid katika mashindano hayo makubwa Ulaya. Modric ni mmoja wa wachezaji bora katika historia ya mchezo huo kutokana na kupita kwake kwa usahihi na maono ya ajabu.

Alikuwa moyo na roho ya safu ya kiungo ya 'Blancos' hao waliposhinda mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa kuanzia 2016 hadi 2018. Pia alipata sifa nyingi za kibinafsi kwa uchezaji wake.

Uwezo wa Modric wa kuamuru muda wa kasi, kudhibiti vita vya katikati ya uwanja na kushawishi mechi muhimu humfanya kuwa mtu bora katika historia ya Ligi ya Mabingwa. Ameshinda Ligi ya Mabingwa mara tano.

### #2 Lionel Messi

Hali ya Lionel Messi kama mmoja wa wachezaji bora katika historia ya Ligi ya Mabingwa haina ubishi. Umahiri wake wa ajabu wa kufunga mabao, ustadi wa kucheza chenga usio na kifani na uthabiti umemfanya kuwa gwiji wa kweli katika mashindano hayo.

Messi anashikilia rekodi nyingi kwenye Ligi ya Mabingwa ikiwa ni pamoja na mabao mengi zaidi ya hatua ya makundi (80), mabao mengi zaidi katika raundi ya 16 (29) na mabao mengi kwa klabu moja (120), yote ambayo yanasisitiza kipaji chake cha hali ya juu.

Ameiwezesha Barcelona kutwaa mataji manne ya Ligi ya Mabingwa katika maisha yake matukufu.

### #1 Cristiano Ronaldo

Cristiano Ronaldo mara nyingi anachukuliwa kuwa mchezaji bora zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa kutokana na rekodi yake ya ajabu ya kufunga mabao na mchango thabiti kwenye mashindano hayo.

Akiwa na mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo amekuwa na mchango mkubwa katika kuziongoza timu zake kupata ushindi.

Rekodi yake ya kufunga mabao mengi zaidi katika historia ya michuano hiyo (140), yakiwamo mabao mengi muhimu katika hatua ya mtoano ni uthibitisho wa uwezo wake wa ajabu.

Uwezo wa Ronaldo wa kutoa katika hali ngumu, pamoja na maisha marefu na uthabiti, imemfanya kuwa na hadhi yake kama mchezaji bora zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



Karim Benzema



Lionel Messi

## Nukuu

"Lazima niwe hapa sasa kusema kwamba haikubaliki, hatukustahili kupoteza mechi. Tunapoteza mechi kwa sababu ya maamuzi ya wazi. Inatia aibu. Aibu. Hiyo ndiyo - fedheha. Huwezi kufikiria ni kiasi gani cha jumbe nilizopata zikisema hii haiwezi kuendelea. Ninapoteza muda wangu. Tunapoteza muda wetu. Sitaki kuwa mikononi mwa watu," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, baada ya VAR kukubali bao pekee la winga wa Newcastle, Anthony Gordon, licha ya kuonekana mpira ulitoka kabla ya kumfikia huku kukiwa na faulo na kuotea.**




"Isiwe mchezo huu tu, hatuwezi kubebwa, lakini mambo yanapokuendea kinyume, wakati mwingine inabidi mkutane na kupigana kama mbwa. Ni kizuizi cha ujenzi na nadhani tulifanya zaidi ya kutosha kushinda mchezo mwishoni," **Kiungo wa Manchester United, Scott McTominay, akizungumzia ushindi wa dakika za majeruhi wa bao 1-0 dhidi ya Fulham juzi.**



"Ulimwenguni. Nilisema hivyo mara nyingi, alipiga shuti zuri kutoka kwa kona fupi na kisha baada ya bao la kwanza, hatua ya bao la pili inaonekana kama Lionel Messi. Nilikumbuka, wakati huo, Messi alifanya hivyo mara nyingi. Labda hiyo ni pongezi nyingi kwake! Lakini anastahili," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akieleza namna winga Jeremy Doku anavyomkumbusha vitu adimu vya Messi, baada ya kufunga bao dhidi ya Bournemouth juzi.**



# HIVI NDIVYO MAKIPA WANAVYOZITESA TIMU LIGI KUU BARA



Golikipa wa Azam FC, Abdulai Iddrisu.

Na Adam Fungamwango

ZIKIWA zimechezwa mechi 55 za Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, kumeonekana makosa ya magolikipa ambayo yanasababisha kujifunga wenyewe, au kusababisha kufungwa mabao ya kizembe wakati mwingine kupoteza mechi.

**Baadhi ya makipa kwenye Ligi Kuu msimu huu, wameonekana kuwa na makosa mengi ambayo yanasababishwa kufungwa mabao rahisi, cha ajabu na kusikitisha ni pale wanapojifunga mabao wenyewe.**

Katika makala haya tumekusanya mabao matano ambayo uzembe wa makipa umechangia 'kuchomesha'....

### 1. Justin Ndikumana (Coastal vs Dodoma Jiji)

Golikipa wa Coastal Union raia wa Burundi ndiye aliyeweka rekodi ya kuwa kipa wa kwanza kujifunga mabao msimu huu kwenye Ligi Kuu. Pia bao alilojifunga ndilo lilikuwa la kwanza kwa mchezaji kujifunga mwenyewe msimu huu.

Agosti 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, kipa huyo akiwa langoni, timu yake ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji FC, alishindwa kuudaka mpira wa krosi ya Raizin Hafiz, mpira ukamponyoka na kujaa wavuni.

Lilikuwa ni bao la kusawazisha kwa Dodoma Jiji iliyokuwa ishapigwa moja kupitia kwa Hija Ugando. Baadaye Meshack Abraham akatumbukiza bao la pili kwa upande wa Dodoma Jiji na kushinda mabao 2-1. Ndikumana asingejifunga, mechi hiyo ingeisha kwa sare ya bao 1-1.

### 2. Abdulai Iddrisu (Azam vs Yanga)

Ni kipa wa kimataifa kutoka nchini Ghana anayeichezea Azam FC. Oktoba 23, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, alifungwa bao linalofanana sana na la Ndikumana wa Coastal Union.

Ilikuwa ni kwenye mechi dhidi ya Yanga, ambapo dakika ya 68 ilitokea faulo nje ya eneo la hatari wakati huo Azam ikiongoza kwa mabao 2-1.

Stephane Aziz Ki alichia shuti ambalo lilikwenda mikononi mwa kipa huyo, lakini kwa mastaajabu ya wengi wakati wakidhani atanyanyuka ili aupige mpira mbele, ulimponyoka na kujaa wavuni, huku mwenyewe akiuongezea kasi kwa kuupiga kichwa katika harakati za kutaka kuuokoa usielekee nyavuni.

Bao hilo lilihesabika kuwa ni la Aziz Ki kwa sababu moja tu, Mburkina Faso huyo alipiga shuti lililolenga lango, vinginevyo angepewa yeye la kujifunga. Raizin wa Coastal hakupewa bao kwa sababu hakupiga langoni, bali ilikuwa krosi.

Mechi hiyo ilimalizika kwa Yanga kushinda mabao 3-2, 'hat-trick' ya Aziz Ki, Gibril Sillah na Prince Dube wakiifungia Azam.

### 3. Mohamed Makaka (Mtibwa vs Geita Gold)

Kipa Mtanzania Mohamed Makaka alikuwa wa pili kujifunga bao msimu huu.

Makaka anayeidakia Mtibwa Sugar alifanya hivyo Oktoba 26, mwaka huu timu yake ikicheza nyumbani, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Ilikuwa ni dakika ya 82, mpira mrefu ulipigwa langoni mwake, akatoka kwenda kuruka kwenye msitu wa wachezaji wake na timu pinzani ya Geita Gold. Nia yake ilikuwa aupangue, lakini nguvu ya mpira ilikuwa kubwa na ikawa ameusukumizia wavuni kwa mikono yake mwenyewe.

Kwa bahati nzuri tu aliwapa Geita Gold bao la kufutia machozi kwani Mtibwa Sugar tayari ilikuwa na mabao matatu kibindoni, hivyo kuondoka na ushindi wa 3-1, mawili ya Seif Karihe na Ladack Chasambi.

### 4. Wilbol Maseke (KMC vs Prisons)

Siku mbili baadaye, Oktoba 28, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kipa wa KMC, Wilbol Maseke akawa kipa wa tatu kujifunga mwenyewe na kuweka rekodi ya aina yake msimu huu.

Kabla ya hapo, hakuna rekodi inayoonesha makipa watatu kujifunga wenyewe kwa msimu mmoja kwenye ligi ya Tanzania.

Dakika ya 53, ulipigwa mpira mrefu ambao ulipigwa kichwa na Edwin Balua wa Prisons. Maseke akiwa peke yake, hajakabwa au kuzingirwa na mtu, alitaka kuupangusa utoke juu ya lango, lakini mpira ulikataa kutii amri, labda kutokana na nguvu ndogo aliyotumia, ukatinga wavuni.

Bahati nzuri, Waziri Junior alisawazisha bao dakika nane kabla mechi kumalizika, timu hizo zikatoka sare ya bao 1-1.


### 5. Ally Salim (Simba vs Ihefu)

Juzi Jumapili, Uwanja wa Benjamin Mkapa, kipa wa Simba, Ally Salim, alifanya uzembe kwa kutemea mpira ndani na kusababisha timu yake kufungwa bao lililokuwa la kusawazisha kabla haijapata la pili kupitia kwa Moses Phiri.

Inashauriwa kwa makipa kutema mipira pembeni, lakini alilipangulia shuti ndani ambapo kwa kawaida ni kama sadaka, mpira unaweza kumkuta mchezaji wa timu yake au pinzani, na ndivyo ilivyokuwa.

Shuti la Rajab Athumani aliyekuwa amepata pasi kutoka kwa Joseph Mahundi, lilipanguliwa kwa mtindo huo na kumkuta miguuni Ismail Mgunda ambaye hakufanya ajizi akaukwamisha wavuni, mechi ikiisha kwa Simba kushinda mabao 2-1.

**JE, WAJUA?**



JUDE Bellingham hadi sasa amefikisha mabao 13 na 'asisti' tatu katika mechi 13 za mwanzo tangu ajiunge na Real Madrid msimu huu. Mabao 10 ya Bellingham ni mara mbili ya mshindi wa Ballon d'Or mara tano, Cristiano Ronaldo, aliyofunga katika mechi zake 10 za kwanza za ligi akiwa na Madrid mwaka 2009.





# Waandishi wanolewa uandishi habari za Bunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu, amewaasa waandishi wa habari za Bunge kujiepusha kutoa habari za upotoshaji zinazosababisha taharuki kwa jamii.

Zungu aliyasema hayo jana kwenye mafunzo ya siku mbili kwa waandishi hao yanayolenga kuwajengea uwezo wa kuripoti habari za Bunge yaliyoandaliwa na Ofisi ya Bunge.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa waandishi kuelewa kanuni, taratibu na miongozo ya uendeshaji shughuli za Bunge ili kuandika habari kwa weledi.

"Vyombo vya habari vimekuwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa shughuli za Bunge, pamoja na uhusiano mzuri uliopo kati ya Bunge na vyombo vya habari, lakini kumekuwa kukijitokeza changamoto ya upotoshaji wa mara kwa mara wa habari zinazohusu Bunge, jambo hili limekuwa kubwa kiasi fulani likichangiwa na kutokuwa na uelewa wa kutosha wa kanuni za kudumu za bunge," alisema.

Alisema kuna wakati waandishi wanashindwa kutofautisha maoni anayotoa mbunge anapochangia hoja na kuchukulia kama ni msimamo wa Bunge.

"Jambo hili si sahihi au wakati fulani kusema Bunge limepitisha Muswada au Azimio fulani wakati halijafikia muda wa kufanya maamuzi, wabunge kuhojiwa na hatimaye hoja kuungwa mkono na waliowengi bungeni," alisema.

Zungu alisema ni vizuri waandishi hao kujielimisha kuhusu uandishi wa habari za Bunge na kusisitiza Ofisi ya Bunge milango ipo wazi kwa jambo lolote litakalohitaji ufafanuzi.

Naye Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, alisema Ofisi ya Bunge imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na vyombo vya habari kuhabarisha umma shughuli zinazofanywa.

"Waandishi wanajengewa uwezo kuhusu kanuni za Bunge, mchakato wa kutunga sheria, upitishaji wa bajeti na uendeshaji wa kamati za kudumu za Bunge, mafunzo haya yanasaidia kuandika habari kwa weledi," alisema.



Naibu Spika, Mussa Hassan Zungu, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo kwa waandishi wa habari wanaoandika habari za Bunge (hawapo pichani), yaliyofanyika ukumbi wa Msekwa bungeni jijini Dodoma mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tanzania kuwa ghala la chakula Bara la Afrika

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TANZANIA inatarajiwa kuwa ghala la chakula katika Bara la Afrika kutokana na mkakati uliowekwa wa kuanza kuzalisha tani milioni moja za mbolea ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo wakati akizindua ghala la kuhifadhia mbolea aina ya Fomi inayozalishwa na Kampuni Intracom Fertilizers Limited.

Alisema mbolea hiyo itazalishwa katika viwanda vitano vinavyojengwa na kampuni hiyo mkoani Dodoma.

Alifanunua kuwa kiwango cha mbolea kitakachozalishwa na kampuni hiyo kitatumika nchini na kingine kuuzwa katika nchi nyingine na kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula Afrika.

"Kuongeza uzalishaji wa mazao, kuondoa umaskini na kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula la Afrika ni maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, viwanda hivi vitakuwa mkombozi kwa Watanzania zaidi ya 3,000 kwa kupata ajira," alisema.

Akizungumzia mbolea ya Fomi inayozalishwa na kampuni hiyo, Serukamba alisema inatunza thamani ya ardhi, uhai wa ardhi kuendelea kuwa kama ilivyokuwa zamani.

"Ukitumia Fomi mfululizo kwa miaka mitatu inawezekana mwaka wa nne usitumie mbolea kwa sababu itakuwa ni nyingi na ardhi yako itaendelea kuwa kwenye thamani ya awali," alisema.

Aliwataka wakulima katika msimu wa kilimo mwaka huu kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kupanua mashamba.

Kuhusu uzalishaji wa alizeti, alisema Mkoa wa Singida umefikia asilimia 50 na lengo ni kufikia zaidi ya asilimia 70 ili kuwa na uwezo wa kulisha nchi nzima.

"Wanasema Singida ni ya tatu kwa umaskini nataka tutoke huko tukianza kazi hii ya kilimo cha umwagiliaji, nina uhakika tutatoka huko kwenye namba tatu ya umaskini," alisema.

Alisema Singida ina miradi 92 inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji yenye mashamba ya ukubwa wa hekta 160,820 ambazo ni zaidi ya ekari 400,000.

Alisema, Singida ni mkoa wa pili nchini kwa kuwa na mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji unaojengwa kwa Sh. bilioni 32 katika Wilaya ya Mkalama.

Awali, Meneja Maendeleo Biashara na Masoko wa Intracom Fertilizers Limited, Dk. Keneth Masuki, alisema mpango wao ilikuwa kujenga viwanda vitatu ili kila kimoja kiwe na uwezo wa kuzalisha tani 200,000 kwa mwaka, lakini kutokana na mahitaji makubwa ya mbolea nchini, serikali iliomba wajenge vitano kuzalisha tani 1,000,000 kwa mwaka. "Kwa taarifa ya Mdhibiti Mkuu wa Mbolea Tanzania (TFRA), Tanzania tunatumia kati ya tani 600,000 hadi 700,000 kwa mwaka, hivyo viwanda hivi vikikamilika vitazalisha tani milioni moja, vitalisha Tanzania nzima na kuwa na ziada ya mbolea ambayo itapelekwa kuuzwa katika soko la nje," alisema.

Masuki, alisema katika kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati kabla ya msimu wa kilimo kuanza, kampuni imefungua maghala ya kuhifadhia katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Singida.

# Mwingiliano binadamu, wanyama chanzo magonjwa kuambukiza

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema kumekuwa na ongezeko kubwa la maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kutokana na mwingiliano mkubwa wa shughuli za kijamii na mwenendo wa mifumo wa maisha na mabadiliko ya hali ya hewa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wadau mbalimbali kwenye ufunguzi wa Kongamano la Kitaifa la Afya Moja lililofanyika jijini hapa.

Mhagama alisema hayo kutokana na takwimu zilizopo duniani matukio yanayojitokeza ya magonjwa ni milioni 100 kila mwaka, inatokana na mwingiliano kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Alibainisha kuwa asilimia 60 ya magonjwa hayo ni ya kuambukiza yanayotoka kwa wanyama na kwenda kwa binadamu,na asilimia 75 ya vimelea vipya vya magonjwa vilivyongunduliwa kwa miongo mitatu asilimia 30 zilitoka kwa wanyama.

Alisema hali hiyo haipaswi kufumbiwa macho bali inatakiwa kushirikiana katika sekta mbalimbali ili kudhibiti matukio hayo.

Kadhalika, kutokana na serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya utendaji na usimamizi wa maafa yanayoathiri afya ya binadamu, wanyama, mimea na mifumo ya ikolojia.

"Serikali kwa upande wake itaendelea kuimarisha usalama ili kupunguza maafa na itaendelea kudhibiti magonjwa ya mlipuko ambayo yanayotokea kwa wandamu na wanyama kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo."

"Ikizingatiwa kuwa magonjwa ya kuambukiza yanasambaa kwa haraka sana kwa wanadamu, wanyama na mimea suala ambalo limekuwa likidumaza ukuaji wa uchumi," alisema.

Waziri Mhagama alizitaka taasisi, mashirika na wadau wa maendeleo, kushirikiana na serikali kutoa elimu kwenye ngazi ya kijamii ili wachukue hatua ya kujilinda na maambukizi ya magonjwa yanayotokana na wanyama na kwenda kwa binadamu.

# NEMC yasitisha uchimbaji dhahabu mgodi Alluvial

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesitisha shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu kwenye Mgodi wa Alluvial Goldmine uliopo Kata ya Ifumbo katika Wilaya ya Chunya kutokana na mwekezaji wa mgodi huo kukiuka sheria ya mazingira kwa kuchimba madini ndani ya mto Zira.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samwel Gwamaka, akiwa na baadhi ya maofisa wa baraza hilo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, maofisa wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Chunya, walifanya ziara ya kushtukiza kwenye mgodi huo unaoendeshwa na Kampuni ya G & I Tech Trading Company LTD kwa lengo la kuangalia kama mwekezaji anazingatia sheria ya mazingira.

Timu hiyo ilibaini kuwa mwekezaji huyo alikuwa anafanya shughuli za uchimbaji ndani ya Mto Zira ambao ni miongoni mwa mito inayomwaga maji kwenye Ziwa Rukwa na kuhatarisha ziwa na viumbe hai.

Dk. Gwamaka alisema awali mwekezaji huyo aliomba kibali cha kusafisha mto huo na kupewa masharti ya kuhakikisha anazingatia usalama wa mazingira ndani ya mto huo.

Alisema walibaini kuwa mwekezaji huyo badala ya kusafisha mto anachimba madini na kujaza vifusi kwenye mkondo wa mto huo na kwenye kingo hali ambayo inasababisha upanuke na udongo kusombwa na maji na kujaza tope kwenye ziwa.

"Kitu cha kwanza tunachokifanya sasa hivi ni kusimamisha shughuli za uchimbaji, lakini hivi vifusi alivyorundika anatakiwa avirejeshe kabla mvua haijaanza kunyesha ili mazingira yarejee katika hali yake ya kawaida, pia atatakiwa kuripoti kwenye ofisi zetu ili aadhibiwe kwa kukiuka masharti," alisema Dk. Gwamaka.

Aliwataka wachimbaji wilayani Chunya kuzingatia taratibu za uchimbaji kwa kuhakikisha wanakuwa na vibali vya Tathmini ya Athari za kimazingira (EIA) kabla hawajaendelea na shughuli zao ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

Mhaidrojia wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa, Nasra Daffa, alisema kwa sasa kina cha Ziwa Rukwa kimeanza kupungua kutokana na kujaa tope linalosababishwa na shughuli za uchimbaji zinazofanyika bila kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Alisema shughuli hizo zinazofanyika ndani ya kingo za mito ni kinyume cha sheria na zinasababisha mito kuhamahama kutokana na udongo na mawe kurundikana kwenye mikondo.

Alisema Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa, imekuwa ikikabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira kwenye mito hiyo kwa kutoa elimu kwa wananchi hasa wachimbaji ambao wanasababisha matatizo zaidi.

"Tunawaomba sana wadau wote watupatie ushirikiano kwenye utunzaji wa rasilimali zetu hizi za maji hasa kwa kuhakikisha tunazuia shughuli za kibinadamu kufanyika ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji ama kwenye kingo za maji," alisema Nasra.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema serikali ya wilaya hiyo inawakaribisha wawekezaji kwenda kuwekeza kwenye shughuli za uchimbaji, lakini wahakikishe wanafuata sheria.

Alisema kwa namna mto huo ulivyoharibiwa kuna uwezekano ukahama njia na kuvamia makazi ya watu kipindi cha masika hali ambayo inaweza ikasababisha maafa.

Wilaya ya Chunya ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa dhahabu katika Mkoa wa Mbeya, lakini baadhi ya wachimbaji wanachimba kiholela na kusababisha uharibifu wa mazingira.

## CCM Mbeya yamwandalia mapokezi Spika Tulia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimemwandalia mapokezi ya kishindo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge Duniani (IPU) kwenye mkutano uliofanyika Jiji la Ruanda nchini Angola.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimishwa kwa kikao cha Kamati ya Siasa ya Mkoa.

Alisema mapokezi hayo yatafanyika Novemba 11, jijini Mbeya wakati Dk. Tulia atakapokuwa anarejea jijini humo akitokea jijini Dodoma.

Aliwataka wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya bila kujali itikadi zao za vyama vya siasa, imani zao wala umri kujitokeza kwenye mapokezi hayo kwa kuchaguliwa kwa Dk. Tulia ni heshima kwa wana Mbeya wote.

"Hata wa vyama vya upinzani tunawaalika kwenye mapokezi hayo kwa sababu huyu sasa ni wa kwetu sote, tunawaalika wazee, vijana, viongozi wa dini, viongozi wa mila na wana Mbeya wote," alisema Mwaselela.

Katika hatua nyingine alisema Kamati ya Siasa ya Mkoa huo iliazimia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa iliyopata miradi mingi ya maendeleo katika kipindi ambacho Rais Samia yupo madarakani ikiwamo ya afya, elimu, kilimo na miundombinu ya barabara.




Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, akipokea msaada wa madawati 491 na mabati 420 yenye thamani ya Sh. mil. 56 kwa Meneja wa NMB Kanda Nyanda za Juu, Straton Chilongola, kwa ajili ya shule saba za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Tunduma, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TUCTA yakerwa migogoro vyama vya wafanyakazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi nchini (TUCTA), limekerwa na ongezeko la migogoro kwenye vyama mbalimbali vya wafanyakazi kwenye mikoa hali inayosababisha kupungua kwa mshikamano miongoni mwa wafanyakazi.

Rais wa TUCTA, Tumain Nyamuhokya, alizungumzia migogoro hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo kwa waajiri wa wafanyakazi ambao ni wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) wa halmashauri zote saba za Mkoa wa Mbeya.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha wakurugenzi watendaji wa halmashauri na maofisa Utumishi wa halmashauri ambao ndio wanahusika na ajira za wafanyakazi wa serikali za mitaa.

Nyamuhokya ambaye ni Mwenyekiti wa TALGWU Taifa, aliwataka wafanyakazi kuachana na migogoro na badala yake washikamane kwenye vyama vyao ili iwe rahisi kupigania haki zao kutoka kwa waajiri wao.

Alisema baadhi ya vurugu zinazotokea zinasababishwa na vyama vyenyewe kugombea wafanyakazi na kusisitiza vyama vyote kufuata taratibu za kupata wanachama kwa kuwasajili wapya badala ya kugombea ambao tayari wana vyama.

Alisema migogoro hiyo inavishushia heshima vyama vya wafanyakazi pamoja na shirikisho na kuwataka wafanyakazi kuacha kuendekeza migogoro hiyo.

"Sisi tunakemea sana hii migogoro kwenye vyama vyetu kwa sababu inatushushia heshima na hadhi zetu kama watetezi wa haki za wafanyakazi, tunaomba vyama vya wafanyakazi vinavyotaka kusajili wanachama visajili ambao hawana vyama," alisema Nyamuhokya.

Akifungu mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa waajiri kwa maelezo kuwa viongozi hao ndio wanaokaa na wafanyakazi muda mwingi na wanatakiwa kuijua vizuri baadhi ya misingi.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia kuimarisha uhusiano kati ya wafanyakazi na waajiri pamoja na kuongeza nidhamu miongoni mwa wafanyakazi.

Alisema wakati mwingine viongozi wa vyama vya wafanyakazi huwa wanaingia kwenye migogoro na waajiri wa wafanyakazi hao kutokana na harakati za kutetea haki na kusimamia sheria hali ambayo alisema mafunzo hayo yataondoa utata unaoibuka.

"Wakati mwingine mnapotetea wafanyakazi mnakuwa sahihi na wakati mwingine mnakuwa hamko sahihi, sasa kinachotakiwa ni ushirikiano kati ya waajiri na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, haya mafunzo ni muhimu sana na nashauri yaendelee kutolewa na kwenye maeneo mengine," alisema Homera.

Baadhi ya waajiri walioshiriki kwenye mafunzo hayo walisema migogoro inayoibuka kwenye vyama vya wafanyakazi inaathiri ufanisi wa kazi miongoni mwao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, Loema Peter, alisema inapoibuka migogoro hiyo waajiri wanajikuta wanatumia muda mrefu kusuluhisha badala ya kufanya kazi na kupunguza ufanisi.

Alisema hata wafanyakazi wanapokuwa na migogoro kwenye vyama vyao wanashindwa kufanya kazi vizuri na kupunguza tija ambayo inatarajiwa na mwajiri.

# Mwinyi kuzindua Taasisi Chuo cha Teknolojia cha India

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, leo anatarajiwa kuzindua Taasisi ya Chuo cha Teknolojia cha India (IIT Madrasa), tawi la Bweleo nje ya mji wa Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu, Lela Muhammed Mussa, alisema chuo hicho ni namba moja nchini India kwa ubora katika fani za TEHAMA.

Alisema Serikali ya Zanzibar imesaini makubaliano na Serikali ya India kuanzishwa kwa tawi la chuo hicho visiwani humo.

Alisema katika makubaliano hayo umiliki wa chuo ni wa Serikali ya Zanzibar, lakini mitaala ya elimu itakayotumika ni ya India na maprofesa 20 kutoka India watafundisha chuoni hapo.

Mitaala itakayofundishwa ni inayotumika India na kwamba Tanzania imeandika historia kwa sababu tangu chuo kianzishwe India miaka 64 iliyopita ndiyo kwanza ifungue tawi nje ya mipaka ya India kwa Afrika.

Alisema uwapo wa chuo hicho ni fursa adhimu na itazidi kujulikana duniani.

Alisema wanafunzi 46 kwa ngazi ya shahada ya kwanza na shahada ya pili wameshaanza kusoma kwa kozi ya data Sayansi na Artificial intelligence na programu hizo ni tunu kwa taifa katika ulimwengu wa teknolojia.

"Tunapokuwa na taasisi kubwa kama hizi itatujengea uwezo sisi wazawa, lakini ni fursa kwa vijana wetu," alisema.


Alisema katika wanafunzi 46 waliojiunga na chuo hicho, 21 ni Watanzania na kati ya hao 21, kutoka Zanzibar ni 17 kati ya wanafunzi wote asilimia 50 wanawake na asilimia 50 wanaume.

Kadhalika, alisema neema hiyo imekuja Zanzibar na ni maendeleo makubwa katika tasnia ya TEHAMA wazawa kupata fursa ya kusoma vyuo vikubwa duniani.

Alisema serikali imepanga eneo la kujenga kampasi kubwa ya chuo hicho huko Fumba na leo Rais Dk. Mwinyi ataweka jiwe la msingi.

Alisema uwapo wa chuo hicho ni fursa nzuri katika kukuza sekta ya utalii kwa sababu wageni wasomi watafika visiwani huo.

Ada ya chuo kwa mwaka ni dola za Marekani 16,000 kwa ngazi ya shahada ya kwanza na dola 8,000 kwa shahada ya pili na wanafunzi wote 17 kutoka Zanzibar wamepata udhamini wa serikali.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, akiteta jambo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, juzi katika hafla ya kusherehekea miaka mitatu ya utendaji kwenye uongozi wake. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Wamabondeni wayahama makazi kwa kujaa maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wanaoishi mabondeni visiwani Zanzibar wamelazima kuyahama makazi yao baada ya nyumba zao kujaa maji kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, alisema mvua imeleta athari kwa baadhi ya maeneo hasa ya mabondeni na nyumba kujaa maji.

Aliyataja baadhi ya maeneo yalioathirika ni Fuoni, Chunga, Tomondo Ziwa Maboga na maeneo mengine katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema awali kabla ya mvua hizo kunyesha serikali ilitoa tahadhari ya kuwataka wanaoishi mabondeni kuhama, lakini baadhi yao walipuuza agizo hilo.

Aliwataka wananchi kutopuuza taarifa zinazotolewa na serikali na Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kuchukua tahadhari mapema.

"Tunashukuru kwamba hadi sasa hakuna madhara ya kifo wala majeruhi yaliyotokana na mvua hii au mafuriko," alisema.

Alisema, athari zingine zilizojitokeza ni kusita kwa baadhi ya shughuli za ujenzi ikiwamo ujenzi wa barabara na uchimbaji wa mitaro. Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ili kuepukana na athari.

Wazazi na walezi pia wametakiwa kuwa na uangalizi mzuri kwa watoto wao ili wasichezee maji yaliotuama.

"Tutahakikishe tunawalinda watoto muda wote, maana watoto wakiona maji yametuama wao ndio hutaka kwenda kuogelea au kutafuta kambare," alisema Mkurugenzi huyo.Tathmini halisi ya nyumba zilizoathirika na mvua haijapatikana.

# Lishe duni yatajwa moja chanzo kuchelewa kuzaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa changamoto ya lishe duni na upungufu wa damu kwa wasichana na wanawake Zanzibar imesababisha kati ya wanawake 10, wanne kutokuwa na uwezo wa kuzaa baada ya kuingia katika ndoa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Kinga Wizara ya Afya, Salim Silim, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema asilimia hiyo imetokana na utafiti wa mwaka 2021/2022 uliofanywa na Tanzania Demographic Health.

Alisema asilimia 47 ya wasichana wanakabiliwa na changamoto ya lishe ya afya zao jambo linalosababisha wanapoingia katika ndoa kupata shida wakati wa ujauzito na kujifungua.

Alisema changamoto hiyo inatokana na vyakula wanavyotumia ambavyo sio vya lishe na kusababisha watoto wa kike kuwapo katika hatari zaidi kuliko wa kiume.

Vile vile, serikali kupitia Wizara ya Afya, inashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar kuhakikisha inatengeneza mfumo wa kupata lishe bora kwa wanafunzi ili kupata jamii bora.

Aliwataka kinababa kuwashajihisha wanawake na watoto wa kike kupata lishe bora, ili kuepusha tatizo la lishe na upungufu wa damu kwa wanawake.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Juma Salim Ali, alisema wanatoa elimu kwa jamii, umuhimu wa kutumia vyakula venye lishe bora ili kuwa na afya bora.

Changamoto kubwa katika jamii ni kushindwa kula vyakula vyenye lishe kutokana na kubadili mifumo ya maisha kwenye vyakula.

"Jamii ni vyema kuachana na vyakula vya mafuta kama chipsi, badala yake kupendelea kula dagaa samaki mboga na matunda," alisema.

Naye Ofisa Lishe, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Zulfat Felision Kabanga, alisema wanatarajia kutoa kinga ya lishe kwa wanafunzi wenye umri wa miaka 12 na kuendelea katika shule zote za serikali za Unguja na Pemba.

Aidha, alisema lishe hiyo ni salama kwa watoto wa jinsia zote kwa lengo la kuwajenga kuwa na siha njema wakati huu na wanapofikia umri wa uzeeni.

# Moto waunguza nyumba, watoto wafariki dunia

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATOTO watatu wa wafugaji katika Kitongoji cha Ruhuma, Kijiji na Kata ya Miruhi wilayani Liwale, mkoani Lindi, wamefariki dunia baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto.

Imeelezwa kuwa nyumba hiyo iliteketea kwa moto wakati watoto hao wakiwa ndani huku wazazi wao wakiwa wamepeleka mifugo machungani.

Ni tukio lililotokea Oktoba 27 mwaka huu saa saba mchana, likithibitishwa na uongozi wa kijiji, kata na Jeshi la Polisi.

Waliofariki dunia ni Damasika Majengo (3), Pendo Majengo (2) na Rungu Majengo (2), wote walikuwa wanaishi Kata ya Mirui wilayani Liwale.

Wakielezea tukio hilo, Dagologofi Beata (22) akiwa na mke mwenza, walidai kuwa siku hiyo waliondoka nyumbani kwao kwenda machungani kupeleka mifugo yao (mbuzi) kwa ajili ya kulisha na kunywesha, watoto wakiwa wamewaacha ndani wakiwa peke yao.

Dagologofi alidai waliporejea saa saba mchana walikuta nyumba yao iliyokuwa imeezekwa kwa nyasi ikiungua huku watoto wakiwa ndani. Moto huo ukasababisha vifo vya watoto wao.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mirui, Chande Mpelembe, alithibitisha kuwapo tukio hilo katika eneo lake la kazi na kubainisha kuwa hawajajua chanzo cha moto huo.

Dk. Salvatory Milanzi wa Zahanati ya Mirui aliyeikagua miili ya watoto hao, alithibitisha vifo vyao vimetokana na kukosa hewa kutokana na mvuke wa moto.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi John Imori alithibitisha kuwa na taarifa za vifo vya watoto hao, huku akiwataka wazazi kuwa makini ikiwa ni pamoja na kutowaacha watoto peke yao.

Alisisitiza lazima awapo mtu mwenye umri mkubwa pale wanapotoka kwenda eneo ambalo ni mbali na nyumba zao.



Mgeni rasmi katika mahafali ya nane ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Rural Development Organization (RDO) Mdabulo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mufindi, Frank Sichalwe, akichangisha fedha kwa ajili ya kusaidia vijana wa chuo hicho ili kuboresha vifaa vyao vya muziki. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Kampuni za kimataifa zajitosa kupunguza uchafuzi mazingira

**Na Halfani Chusi**

KUKABILIANA na athari za uchafuzi wa mazingira utokanao na kemikali za bidhaa za majokofu na viyoyozi, kampuni za kimataifa Toshiba na Carrier zimezindua bidhaa mpya zitakazosaidia kupunguza athari hizo.

Vilevile viongozi wa kampuni hizo wameishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwakaribisha kuwekeza nchini, wakibainisha kuvutiwa na mazingira ya uwekezaji nchini.

Katika uzinduzi wa bidhaa hizo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Ajay Kumar Garg, Meneja wa Kanda ya Afrika wa AHI Carrier yenye maskani yake Dubai, alisema bidhaa zao zina kiwango kidogo cha Fluorine - gesi ambayo ni hatari kwa afya na mazingira huku bidhaa zao zikitumia kiwango kidogo cha nishati kulinganishwa na bidhaa za sasa.

Alisema bidhaa hizo zimeundwa kufanya kazi ya majokofu ya R32 na zina teknolojia kamili ya inveta inayotoa kiwango cha juu cha ufanisi wa nishati.

Alisema majokofu hayo yametengenezwa ili kupunguza athari za mazingira, wakienda sambamba na jitihada za kimataifa za kukabiliana athari za mabadiliko ya tabianchi.

Meneja huyo alisema bidhaa zilizozinduliwa zinatoa mchango zaidi katika maisha ya soko la Afrika na kuokoa nishati zaidi na kulinda mazingira.

"Tumezingatia mzunguko wa maisha ya uendeshaji, si tu vifaa vyetu, bali pia baada ya makabidhiano ya vifaa ni kwa kiasi gani mteja anaweza kunufaika na uimara na kuokoa fedha za matengenezo," alisema.

Subrata Biswas, Meneja Mauzo Afrika Mashariki wa AHI Carrier, alisema bidhaa zao zinatumia nishati kidogo kwa lengo la kupunguza bili ya umeme kwa watumiaji.

Toshihiro Yamamoto, Meneja Mkuu wa Toshiba alisema usumbufu wa kiyoyozi kwa sasa si lazima, akifafanua "ni hitaji leo na kwa kuwa hitaji hili lipo, tunahitaji kuwa hapa na teknolojia za hali ya juu."

Aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwapa ushirikiano mkubwa kiuwekezaji, akibainisha kuwa wamepokewa vyema Dar es Salaam na Dodoma.

"Kiyoyozi si tu juu ya kudhibiti halijoto. Inabidi tufanyie kazi suluhu za kiubunifu ambazo tunaweza kuokoa nishati, kupunguza gharama, si tu kwa mtumiaji, bali pia kwa serikali, kwa sababu uzalishaji wa nishati ni changamoto ulimwenguni," alisema.

# Morogoro kuongeza uzalishaji wa sukari

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UONGOZI wa Mkoa wa Morogoro umejipanga kuchangia asilimia 75 ya uzalishaji wa sukari nchini ifikapo mwakani baada ya kuhamasisha wawekezaji kupanua viwanda vya sukari na kujenga vipya.

Mikakati ya kuongeza uzalishaji huo inatokana na kuwapo mazingira wezeshi yanayotolewa na serikali ambayo yamewavutia wawekezaji na kuwafanya kujiamini kuwekeza zaidi katika mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliyasema hayo jana katika programu ya mikutano ya wakuu wa mikoa, wakurugenzi wa halmashauri na vyombo vya habari.

Programu hiyo inatoa fursa kwa viongozi hao kuelezea utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo katika mikoa na halmashauri zao inayotokana na fedha zinazotolewa na serikali kuu.

Malima alisema Mkoa wa Morogoro unashika nafasi ya kwanza katika uzalishaji sukari nchini kutokana na kuendana na kilimo cha miwa. Uzalishaji sukari ni zaidi ya tani 450,000 katika viwanda vya mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa alisema uzalishaji huo wa zaidi ya asilimia 75 ya sukari yote itakayozalishwa nchini utatokana na kukamilika kwa ujenzi na upanuzi wa viwanda vipya vitatu vya sukari vya Kilombero, Mtibwa na Mkulazi vilivyomo mkoani humu.

"Kwa sasa uwekezaji unaoendelea kwenye sekta ndogo ya sukari utaifanya nchi yetu ijitosheleze kwa sukari," alisema.

Malima aliipongeza serikali kwa kuweka sera nzuri na mazingira wezeshi ya uwekezaji ambayo yamewafanya wawekezaji kujiamini kuwekeza nchini.

"Mazingira mazuri yanayofanywa na serikali yamechangia sasa uwekezaji mkubwa kwenye viwanda hivi na kuwezesha taifa kujitegemea kwenye bidhaa ya sukari," alisema.

Malima alisema Kiwanda cha Mtibwa kimewekeza zaidi ya Sh. bilioni 100, pia kuna uwekezaji katika Kiwanda cha Mkulazi kitakachozalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka pamoja na uwekezaji wa kiwanda kipya cha Kilombero kitakachozalisha tani 200,000.

"Karibu theluthi moja ya mahitaji yote za sukari nchini inazalishwa Kilombero na haya si ambayo yanajitokea tu, bali ni mipango mizuri ya serikali na Morogoro inajivunia kuwa mfano mpana wa mafanikio ya serikali," alisema Malima.

SIKU 30 ZA GAZA:



Baadhi ya familia zikiwa katika moja ya shule Ukanda wa Gaza, kujihifadhi kwa makazi kutokana na mashambulizi yanayoendelea nchini humo. **PICHA: UN**

# UN: Makazi, vituo vimejaa kupita kiasi

**Na Christina Mwakangale**

NI takribani siku 30 tangu eneo la Gaza lilipoanza kupokea mashambulizi ya kijeshi ikitokana na kikundi cha Hamas kuwashambulia Waisrael, Oktoba 7, mwaka huu, kusini mwa Israel na kusababisha vifo takribani 1,400.

Tangu mashambulizi hayo mamlaka ya Palestina inasema takribani Wapalestina 9,000 wamepoteza maisha miongoni mwao zaidi 3,000 ni watoto, wakiwamo wanawake na wazee na takribani watu milioni 1.5 wameyakimbia makazi yao.

Mamlaka ya jeshi la Israel inasema takribani mateka 200 wanashikiliwa na Hamas huko Gaza, licha ya juhudi za kimataifa kusitisha wito wa aina tofauti ikiwamo kusitishwa kwa mgogoro huo, kuachiliwa mateka pamoja na ulinzi wa raia.

Kumekuwapo pia na maandano kwenye miji tofauti ikiwamo nchi za kiarabu, huku waandamanaji wakisisitiza kusitishwa kwa mgogoro huo na katika mji wa Telaviv wakidai kuachiliwa kwa mateka.

Kwa mujibu wa televisheni ya BBC, Waziri wa Mambo ya Nje ya Marekani, Anthon Blinken, aliwasili nchini Jordan kwa ajili ya mazungumzo ya kidiplomasia hususan kwa nchi za kiarabu. Kadhalika jana alitarajiwa kuwasili Uturuki kwa shughuli hiyo.

Blinken, akiwa Mashariki ya Kati alikutana na Kiongozi wa Mamlaka ya Palestina Mahmoud Abbas, wakizungumza mgogoro huo, uliodumu kwa takribani mwezi mmoja. Blinken amewasili katika makao makuu ya Mamlaka ya Palestina katika Ukingo wa Magharibi na kukutana na Abbas.

Abbas, pia anajulikana kama Abu Mazen, amekuwa kiongozi wa Mamlaka ya Palestina (PA) tangu 2005 na anawakilisha chama cha kisiasa cha Fatah, mpinzani mkali wa Hamas, ambayo inaendesha Gaza.

Palestina inasimamia sehemu za Ukingo wa Magharibi ambazo haziko chini ya udhibiti kamili wa Israel.

> “Ombi la awali la dola milioni 294 la kusaidia takribani watu milioni 1.3 liliwasilishwa Oktoba 12, mwaka huu, lakini halitoshelezi, amesema Laerke.



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, akiwa na kiongozi wa Mamlaka ya Palestina, Mahmoud Abbas, baada ya kuwasili ulingo wa Gaza, jana. **PICHA: BBC**

**UN**

Shirika la Umoja wa Mataifa (UN), linalosimamia amani, jana limesema kwamba watu milioni 1.5 huko Gaza wamekimbia makazi yao na vituo kwa ajili ya kuwatunza vimejaa kupita kiasi.

Zaidi ya wakimbizi wa ndani 710,000 wanapewa hifadhi katika vituo vinavyosimamiwa na UNRWA, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina, huku hofu ikisalia kuwa ni hatari kubwa za kiafya na ulinzi.

Shirika hilo linasema, takribani watu 530,000 wanahifadhiwa katika maeneo 92 ya UNRWA kusini mwa Gaza na malazi yakizidi uwezo na kwamba sasa haliwezi kupokea wageni wapya. Watu wengi waliokimbia makazi yao wanalala mitaani karibu na vituo vya UNRWA.

Kadhalika, Kaskazini mwa ukanda wa Gaza, takribani watu 160,000 wamehifadhiwa katika vituo vya UNRWA, licha ya shirika hilo kueleza kwamba halina uwezo wa kuwapatia huduma tena, kutokana na kukosa taarifa sahihi kuhusu mahitaji ya watu.

Jens Laerke, kutoka wa ofisi ya Umoja wa Mataifa ya kuratibu misaada ya kibinadamu na dharura (OCHA), hivi karibuni akizungumza na waandishi wa habari Geneva, Uswisi, amesema wiki hii, UN na wadau watatoa ombi la fedha za kusaidia eneo linalokaliwa la wapalestina, kwa ajili ya kipindi chote cha mwaka kilichosalia.

Ombi la awali la dola milioni 294 la kusaidia takribani watu milioni 1.3 liliwasilishwa Oktoba 12, mwaka huu, lakini halitoshelezi, amesema Laerke.

Hivi sasa watu milioni 2.7, sawa na idadi ya watu wote Gaza na watu wengine 500,000 katika eneo linalokaliwa la Ukingo wa Magharibi wanahitaji msaada wa chakula, maji, huduma za afya, malazi, huduma za kujisafi na kwamba gharama ya kukidhi mahitaji yote hayo ikikadiriwa kuwa dola bilioni 1.2.

Laerke amesema ombi la kwanza limefadhiliwa kwa asilimia 25 hadi sasa na kwamba wafadhili wakuu ni Marekani, Japan na Mfuko wa UN wa usaidizi wa dharura (CERF), wenye wafadhili kutoka maeneo mbalimbali.

Anatoa wito wa sitisho la mapigano kwa minajili ya kuwezesha misaada ya kibinadamu kufikia walengwa, akisema hatua kama hiyo imewezekana Kaskazini-Magharibi mwa Syria, Yemen na Afghanistan.

Mazungumzo ya kidiplomasia yanaendelea yakihusisha Israel, Misri, Marekani na UN, huku zaidi ya malori 300 yakiwa na misaada yameingia Gaza hadi kufikia Novemba 2, mwaka huu.

Zaidi ya malori 100 yaliingia Gaza, hadi tarehe hiyo pekee, ikiwa ni idadi ya chini sana ya malori 500 ya mizigo ambayo yalikuwa yanaingia Gaza kila siku kabla ya mgogoro kuanza Oktoba 07, mwaka huu.

**IMEANDALIWA KWA MSAADA WA MTANDAO**

# SIMBA, YANGA ZAIPONZA IHEFU KWA AZAM LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Bruno Ferry (pichani), amesema mfumo wa kuchezesha mabeki watatu nyuma bila ya kuwa na mshambuliaji mbele badala yake kujaza viungo ndiyo uliosababisha kupata ushindi mnono dhidi ya Ihefu kwenye uwanja wake wa nyumbani, huku beki Lusajo Mwaikenda akisema walimu wao waliifuatilia timu hiyo kwenye michezo iliyocheza dhidi ya Yanga na Simba.

Akizungumza baada ya kumalizika mechi hiyo juzi, katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya, Azam ikishinda mabao 3-1, kocha huyo alisema waliingia na mfumo huo kwa asilimia 100 kipindi cha kwanza na kuwachosha kabisa wapinzani wao, kabla ya kubadilika kidogo kipindi cha pili na kumaliza mchezo.

**"Tulianza na mabeki watatu nyuma, hatukuwa na straika mbele, tukajaza viungo wengi kati kwa ajili ya kumiliki sana mpira na kuwachosha na walichoka kweli, kipindi cha pili tulibadilika kidogo tu tukapata mabao mawili, ndiyo maana utaona mabao yetu yote matatu yamefungwa na viungo," alisema Bruno.**

Yalikuwa ni mabao mawili ya kiungo mkabaji, Sospeter Bajana na moja la kiungo mshambuliaji, Feisal Salum, huku bao la kufutia machozi la Ihefu likipachikwa nyavuni na Jaffar Kibaya.

Beki wa Azam, Lusajo alisema makocha wao waliwasoma vizuri Ihefu kwenye michezo yao iliyopita na hasa dhidi ya Yanga na Simba na kuangalia aina ya mpira wanaocheza na jinsi gani ya kuwadhibiti.

"Tuliwasoma vizuri tu, uzuri wao na mapungufu, makocha wakapanga mifumo yao, wakatuambia wachezaji jinsi gani ya kwenda kuyatumia madhaifu yao uwanjani," alisema Lusajo.

Kocha Mkuu wa Ihefu, Mganda, Moses Basena, alisema waliruhusu bao moja kipindi cha kwanza na wakaruhusu mawili kwa dakika zilikaribiana ambayo yaliwavunja nguvu wachezaji wake.

"Inabidi turekebishe sana safu ya ulinzi naona ina shida," alisema Basena.

Azam imefikisha pointi 19, huku Ihefu ikiwa na pointi zake nane.




MABINGWA...




Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mntenjele, akisaidiana na viongozi mbalimbali wa wilaya hiyo kukabidhi kombe kwa Nahodha wa Kewanja FC, Geofrey Emmanuel, baada ya kuibuka mshindi kwenye mechi ya fainali ya michuano ya Barrick North Mara Mahusiano Cup 2023, kwa kuichapa Kerende FC bao 1-0 katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Ingwe, wilayani Tarime juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# KMKM yapotea tena, yajipa matumaini

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

PAMOJA na kupoteza mchezo wa tatu msimu huu, Kocha Msaidizi wa KMKM SC, Ame Msimu, amesema licha ya matokeo hayo bado hayajarudisha nyuma jitihada zao za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, juzi waliendelea kupunguzwa kasi ya kutetea taji hilo baada ya kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Maafande wa Zimamoto SC katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri.

Mabao ya Maafande wa Zimamoto yalipachikwa nyavuni na Hussein Mwinyi dakika ya 30 na Hussein Abdallah dakika ya 60.

Kwa matokeo hayo KMKM inakuwa imepoteza jumla ya michezo mitatu kati ya tisa iliyocheza hadi sasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Msimu alisema licha ya matokeo hayo bado hayajawarudisha nyuma jitihada zao za kutetea ubingwa wanaoshikilia baada ya kuutwaa msimu uliopita.

Alisema wataendelea kukisuka kikosi chao ili kufanya vizuri katika michezo sita iliyobaki ya kukamilisha mzunguko huu wa kwanza wa ligi hiyo.

Kuhusu mchezo huo, alisema makosa madogo yaliyofanywa na walinzi wake ndio yaliyosababisha kufungwa katika mchezo huo.

Alisema siku zote wanapokutana na timu ya Zimamoto, mchezo huo huwa mgumu kwa pande zote, hivyo hawezi kutupia lawama wachezaji wake kwa sababu walicheza vizuri.

"Tulicheza vizuri katika dakika zote 90, licha ya kufungwa bao la kwanza dakika za mapema, wachezaji walijituma sana ili kuweka mambo sawa, lakini pengine haikuwa bahati yetu,"alisema.

Kwa matokeo hayo KMKM imeshuka hadi nafasi ya tatu ikitokea nafasi ya pili ikibaki na alama zake 16 wakati Zimamoto wakipaa kutokea nafasi ya nne mpaka ya pili na pointi zao 17.

Kwa upande wa kinara wa ligi hiyo, timu ya JKU, imeendelea kujiimarisha kileleni kwa kufikisha alama 20 baada ya hiyo juzi kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Ngome FC katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Mau B saa kumi alasiri.

# KMC FC yataja uchovu sababu kichapo Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa KMC FC, John Matambala, amesema uchovu wa kucheza mechi kila baada ya siku mbili ndio uliochangia kichapo dhidi ya Dodoma Jiji.

Amesema kwa sasa kazi kubwa wanayoifanya wao kama makocha ni kuwaandaa wachezaji wake kuwa tayari kucheza mechi mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara.

KMC FC katika michezo tisa waliyocheza wameshinda minne, sare tatu na kuchezea kichapo mara mbili ikiwa ni pamoja na mchezo wao wa Ijumaa iliyopita ambao walikubali kulala kwa mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji FC, hivyo hadi sasa kujikusanyia jumla ya pointi 15.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema wachezaji walipambana katika mchezo huo, lakini walishangazwa kwa kichapo kutokana na kucheza kwa uchovu hivyo kuruhusu bao la mapema katika kipindi cha kwanza.

Alisema kuwapo kwa fatiki na uchovu wa kucheza mechi kila baada ya siku mbili ndiko kulikochangia kupoteza mchezo huo uliopigwa katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Matambala (pichani chini) alisema: "Nawapongeza wachezaji kwa kupambana katika michezo tuliyocheza, baada ya kupoteza dhidi ya Dodoma Jiji FC tumerudi uwanja wa mazoezi kuongea na wachezaji wetu kuwaandaa kiakili na kimwili kukabiliana na mechi za mfululizo.

"Lakini pia kuna makosa tumefanya na kuadhibiwa jambo hilo tunaenda kulifanyia kazi na kujiandaa na mchezo wetu ujao dhidi ya Kagera Sugar," alisema kocha huyo.

Alisema kulingana na mechi yao ijayo dhidi ya Kagera Sugar kucheza Novemba 27, mwaka huu wanatatumia muda huo kufanyia kazi makosa yao na kujiandaa vizuri ili kuendelea kukusanya alama ugenini kama ilivyo kwa michezo yao miwili iliyopita.

Aliongeza kuwa anaimani kubwa ya kuweza kupata matokeo ugenini dhidi ya Kagera Sugar kwa sababu mechi saba walifanikiwa kucheza mbili ugenini na kuvuna alama nne wakishinda 2-1 dhidi ya Geita Gold FC na kutoka Suluhu na Tabora United.



## ZISIKUPITE

### WIRTZ AWINDWA LIVER

LIVERPOOL ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, 20. ***(Star)***

### ANTONY, BARBOSA KUPISHANA

KLABU ya Manchester United ipo tayari kumtoa ofa mlinzi wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 23, katika mkataba wa kubadilishana mshambuliaji mwenye umri wa miaka 27, Gabriel Barbosa kutoka Flamengo. ***(Mirror)***

### PHILLIPS ALENGWA JUVE

KIUNGO wa kati wa England na Manchester City, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27, ameibuka kuwa mchezaji anayelengwa na Juventus Januari. ***(Mail)***

### MUSIALA AWINDWA MADRID

KLABU ya Real Madrid itamwinda kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20, ikiwa hawataweza kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe kutoka Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 24. ***(ESPN)***

### MESSI AIKATAA BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 36, amekataa kurejea Barcelona kwa mkopo baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu ya Marekani, MLS. ***(Mail)***

### FELLAINI YUPO HURU

KIUNGO wa zamani wa Ubelgiji na Manchester United, Marouane Fellaini mwenye umri wa miaka 35, ni mchezaji huru baada ya kuondoka katika Klabu ya China ya Shandong Taishan. ***(Fabrizio Romano)***

### DAVIES KUTUA MADRID

KLABU ya Real Madrid pia inakaribia kumnunua beki wa kushoto wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 23, Alphonso Davies. ***(AS)***

### WATKINS MSHAHARA MNONO

MSHAMBULIAJI wa England, Ollie Watkins mwenye umri wa miaka 27, atakuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi Aston Villa baada ya kuafiki mkataba mpya wa pauni 150,000 kwa wiki. ***(Football Insider)***

### EZE KUONGEZEWA MSHAHARA

MSHAMBULIAJI wa England, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 25, ataongeza mshahara wake mara tatu kwa mkataba mpya na Crystal Palace ambao itakuwa na kipengele kikubwa cha kuachiwa. ***(Teamtalk)***

### KIMMICH AWANIWA BARCA

BARCELONA ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, akiwa hana matumaini ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Fichajes)***

### PAU NA DILI LA MADRID

MLINZI wa Aston Villa na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 26, amesema alikuwa karibu kujiunga na Real Madrid kutoka klabu ya zamani ya Villarreal msimu wa 2021. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MADRID YAKANA KUTETA NA MBAPPE USAJILI UJAO

**PARIS,** Ufaransa

**Habari hizi ni za uongo kabisa na mazungumzo yaliyosemwa na mchezaji ambaye...**

REAL Madrid imekanusha kufanya mazungumzo na Kylian Mbappe kuhusu kumnunua mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain msimu ujao wa majira ya joto.

**Klabu hiyo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, ilikanusha ripoti iliyosema kwamba mazungumzo yamefanyika na kusema ni "uongo kabisa" katika taarifa iliyotolewa jana.**

"Mbele ya habari zinazotangazwa na kuchapishwa na vyombo mbalimbali vya habari, ambavyo vinakisia kuhusu mazungumzo yanayodhaniwa kuwa kati ya mchezaji Kylian Mbappe na klabu yetu, Real Madrid inataka kusema kwamba habari hizi ni za uongo kabisa na mazungumzo yaliyosemwa na mchezaji ambaye ni wa PSG hayajafanyika," ilisema taarifa ya Real Madrid.

Gazeti la Marca - katika habari yake ya ukurasa wa mbele Alhamisi - liliripoti kwamba "Madrid wanakaa kimya, lakini klabu inamwona akiwa amevaa nguo nyeupe mwaka 2024."

Gazeti la Ufaransa L'Equipe liliandika Ijumaa kwamba Madrid "bado wanamngoja Mbappe," wakati Jumamosi Diario AS iliripoti kwamba fowadi huyo angetarajia kupata euro milioni 35 kwa mwakani akitua Bernabeu.

Mbappe amekuwa akilengwa sana na Madrid na rais wa klabu Florentino Perez kwa muda mrefu.


Miamba hao wa LaLiga walishindwa kumsajili Mbappe mwaka 2021 - walipowasilisha ofa ya euro milioni 200 siku ya mwisho ya uhamisho, ambayo ilipuuzwa na PSG - na mwaka 2022, wakati walikuwa karibu kumpata kwa uhamisho wa bure kabla ya yeye kuamua kusaini mkataba mpya Paris.

Madrid walihusishwa tena na Mbappe msimu uliopita wa majira ya joto alipotangaza kwamba hatasaini nyongeza ya PSG, ikimaanisha kuwa atakuwa huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine Januari 2024 kabla ya kuhama msimu wa maji ya joto.

Klabu hiyo ya Hispania iliacha jezi namba tisa ikiwa wazi kwa msimu wa 2023-24 na badala yake wametegemea mabao ya Jude Bellingham.

Mbappe amefunga mabao 10 katika mechi 10 za Ligue 1 akiwa na PSG hadi sasa msimu huu, na mawili katika mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# HERNANDEZ AKERWA NA KIWANGO BARCELONA



**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez, alitaja uchezaji wa Barcelona dhidi ya Real Sociedad kuwa haukubaliki na akalaumu matokeo ya El Clasico licha ya kushinda bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Reale Arena.

Ronald Araujo alifunga kwa kichwa bao pekee la ushindi dakika ya 92 na kubeba pointi tatu baada ya mechi iliyokuwa imetawaliwa kwa sehemu kubwa na wenyeji.

Xavi alikiri kwamba Sociedad walistahili zaidi kwa uchezaji wao na alikosoa uchezaji wa timu yake, akisema wachezaji bado walikuwa wamelewa na kichapo cha mabao 2-1 wiki iliyopita kutoka kwa Real Madrid.

"Dakika 25 za kwanza hazikubaliki," alisema kocha huyo wa Barca katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo.

"Ni kinyume na wiki iliyopita, tulipocheza vizuri na tulistahili kushinda, lakini tukashindwa. Leo (juzi) ni siku ya kujikosoa sana.

"La Real ni timu nzuri na walionesha nguvu zaidi kuliko sisi. Hatukuwa na raha hata kidogo. Tulikuwa na 'hangover' kutoka El Clasico. Tuliathiriwa zaidi na matokeo hayo kuliko nilivyofikiria."

"Wakati wa mapumziko, niliwauliza wachezaji kama walikuwa wamechoka na wakaniambia hawakuwa wamechoka," aliongeza Xavi.

"Kwa hivyo, niliwaambia wanapaswa kucheza kwa nguvu zaidi. Ilikuwa rahisi kama hiyo.

"Kipindi cha pili tulikuwa bora zaidi. Sare haitoshi kamwe. Tulifanya mabadiliko ya kushambulia na kushinda mchezo na kumaliza kwa nguvu.

"Tulikuwa vizuri katika dakika 10 za mwisho. Timu ilijisikia vizuri zaidi na tukatengeneza nafasi, Gavi akikaribia na kisha Ronald kupata bao.

## Kane ajiwekea rekodi Bundesliga

**MUNICH,** Ujerumani

HARRY Kane alifunga hat-trick wakati Bayern Munich ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Borussia Dortmund na kumfanya mchezaji huyo wa Kimataifa wa England kuvunja rekodi ya muda wote ya kuwa na mabao mengi zaidi katika mechi 10 za kwanza za Bundesliga kwa mchezaji huyo, akiwa amezifumania nyavu mara 15.

Bayern walianza kwa kasi katika Uwanja wa Signal Iduna Park, huku Dayot Upamecano akiunganisha kwa kichwa kona ya Leroy Sane dakika ya tano.

Winga huyo wa zamani wa Manchester City, kisha alitengeneza la pili katika dakika ya tisa, akicheza pasi ya uhakika kwenye eneo la yadi sita kwa Kane aliyefunga bao la pili.

Baada ya mapumziko, krosi ya Kingsley Coman ilimpata Kane kwa bao la tatu kabla ya mshambuliaji huyo huyo kukamilisha hat-trick yake dakika za mwisho za mchezo huo.

Ni mara ya tatu katika rangi za Bayern kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kufunga mabao matatu tangu ajiunge nayo Agosti mwaka huu akitokea Tottenham Hotspur.

Baada ya mechi, Kane alizungumzia umuhimu wa ushindi kwa vijana hao wa kocha Thomas Tuchel.

Aliiambia Bundesliga.com: "Ulikuwa mchezo mzuri sana wa pande zote.





## Arteta alia na bao la Newcastle United

**LONDO,** England

MIKEL Arteta alisema bao la ushindi la Anthony Gordon katika ushindi wa 1-0 wa Newcastle United dhidi ya Arsenal lilikuwa "fedheha kabisa" na "aibu" kwa Ligi Kuu England.

Bao la Gordon la dakika ya 64 Jumamosi lilitolewa na mwamuzi Stuart Attwell baada ya ukaguzi mara tatu wa VAR ili kutathmini kama Joelinton alifanya madhambi kwa kumsukuma beki Gabriel na kama Gordon alikuwa ameotea.

Baada ya kusubiri kwa muda mrefu ukaguzi ukamilike kupitia VAR, bao la Gordon lilitolewa na Newcastle wakashikilia kupata ushindi huo na kuwapa Arsenal kipigo chao cha kwanza cha Ligi Kuu England msimu huu.

Akizungumza katika mkutano na wanahabari baada ya mechi, Arteta alikasirishwa na uamuzi huo.

"Inashangaza, lazima tuzungumze juu ya matokeo," alisema Arteta.

"Lazima tuzungumze jinsi lengo hili linasimama, naona aibu. Ni aibu kabisa bao hili linaruhusiwa. Si bao - kwa sababu nyingi.

"Ili bao kuruhusiwa, kuna mambo fulani kabla ya hapo, kuna mambo hayaruhusiwi katika soka, hapa au China au Japan au Ureno."

Matumizi ya VAR ya Ligi Kuu England yamekosolewa vikali kufuatia mfululizo wa matukio ya kutatanisha msimu huu.

Arteta alisema mchakato wa uamuzi wa bao la Newcastle ni mfano mwingine wa Ligi Kuu kuharibiwa na tafsiri yake ya VAR.

"Kuna mengi hatarini, ni ngumu sana kushindana katika kiwango hiki," alisema Arteta. "Ni aibu. Nimekaa zaidi ya miaka 20 katika nchi hii na haipo karibu na kiwango cha ligi bora duniani.

"Sijali wanachosema. Tumechelewa. Lazima nisimame hapa na kueleza. Tumepoteza pointi tatu. Kuna mengi sana hatarini, inatia aibu."

Meneja wa Newcastle Eddie Howe, pamoja na kusema anaamini ni bao zuri, alikiri kwamba mchakato wa uamuzi huo haukuwa wazi.

"Tuko gizani," Howe alisema. "Tumesimama kando ya uwanja tukiona VAR kwenye 'skrini' lakini bila picha.

"Sijaona chochote zaidi ya kile nilichokiona wakati huo. Lilionekana kuwa bao zuri kwangu."



# MGUNDA AITAKA SIMBA QUEENS KUWAHI KAMBINI

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba Queens kinachonolewa na Juma Mgunda, kinatarajia kuingia kambini kesho kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake inayotarajiwa kuanza Desemba, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Simba Queens, Seleman Makanya, alisema timu yao inaingia kambini kujiandaa na msimu mpya wa ligi hiyo, ambapo wamedhamiria kufanya kweli ili kurejesha heshima ya klabu hiyo kuwania ubingwa wa Ligi Kuu.

"Tunatarajia kuingia kambini Jumanne, tulikutana kwa kufanya kikao na Kocha Mkuu (Mgunda) kwa ajili ya mipango yetu ya msimu ujao na kuona kuanza kuingia kambini mapema na kuendelea maandalizi ya msimu mpya.

**"Bado hatujajua ratiba kwa sababu kesho (leo), tunatarajia kukutana na viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kuona mchakato wa ratiba tunaanza na nani na wapi," alisema Makanya.**

Aliongeza kuwa msimu huu wamefanya usajili mzuri kwa kuongeza nguvu kwenye mapungufu yaliyojitokeza msimu uliopita na wana uhakika wa kufanya vizuri katika mechi zao kufikia malengo ya kurejesha heshima ya klabu hiyo kutwaa ubingwa.

Makanya alisema ni mapema kuzungumzia wanachukua ubingwa kwa sababu bado hata ratiba hawajaiona, lakini moja ya mikakati yao ni kuona timu yao inafanya vizuri kila mechi na kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

## *TMA nayo yaiengua Kengold kileleni Ligi ya Championship*

**Na Adam Fungamwango**

KINACHOENDELEA kwenye Ligi ya Championship ni vita ya kunyang'anyana usukani, baada ya TMA nayo wiki hii kuiondoa Kengold kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo iliyoendelea juzi kwenye viwanja mbalimbali nchini.

Kengold ya Mbeya iliyokuwa ikiongoza ligi hiyo tangu wiki iliyopita, ililazimishwa suluhu nyumbani, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Stand United na kufikisha pointi 20 sawa na Mbeya Kwanza ambayo nayo ilifikisha idadi hiyo ya pointi kwa kuifunga Copco mabao 2-1, Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

Wakati hayo yaliendelea, TMA ya Arusha, ikiwa ugenini, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, iliidungua Transit Camp bao 1-0 na kupanda kileleni mwa msimamo ikifikisha pointi 21, ikizipiku Kengold ambayo imeshuka hadi nafasi ya pili ikiwa na mabao mengi dhidi ya Mbeya Kwanza ambayo ipo nafasi ya tatu katika msimamo huo.



Mashabiki wa Yanga wakishangilia ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga ipewe maua yake kuikanda Simba 5G*

INATOKA UKURASA 24

na la nne kwa upande wa Yanga, akimalizia kwa ulaini mpira wa krosi iliyochongwa na Clement Mzize ambaye alimuacha kwa mbio, Mohamed Hussein 'Tshabalala' kabla ya kumuweka mfungaji.

Msumari wa mwisho kwenye kwa Simba uligongelewa na Pacome kwa mkwaju wa penalti, dakika tano kabla ya mechi kumalizika. Penalti hiyo ilitokana na Inonga kumkwatua Nzengeli ndani ya eneo la hatari na mwamuzi Ahmed Aragija akaamuru tuta, lililowekwa wavuni na Muivoy Coast huyo.

### KABLA YA MECHI

Licha ya Dar es Salaam kubinkwa na mvua haikuweza kukwamisha mashabiki wa timu hizo mbili kushindwa kuja uwanjani na kuanza kuingia tangu saa 4:00 asubuhi bila kujali kulowana.

Shamra shamra za mchezo huo zilianza mapema kwa kuwapo kwa burudani za kigoma kupigwa uwanjani kabla ya kuanza kwa mchezo huo.

Hali ya usalama ilikuwa ya juu vyombo vya ulinzi na usalama vilikuwa kila mahala kuhakikisha mashabiki waliojitokeza uwanjani wanapata burudani bila bughuza.

### TIMU KUWASILI

Timu ziliwasili uwanjani saa 9:00 na dakika 17 baadaYe wachezaji wa Yanga walikuwa wa kwanza kuingia kwenye dimba kwa lengo la kukagua uwanja walifanya hivyo takriban dakika 15 na baadaye kurejea vyumbani.

Saa 9:43 benchi la ufundi la Simba likiongozwa na Kocha Msaidizi Ouanane Sellami waliingia dimbani kupanga koni za kwa ajili ya wachezaji kutoka vyumbani na kupasha misuli moto kabla ya mechi kuanza.

Baada ya dakika 23 (saa 10:06) wachezaji wa Simba waliingia uwanjani kwa ajili ya kupasha misuli huku nyota watatu wa Wekundu Msimbazi hao, Henock Inonga, Ally Salim, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Jean Baleke wakienda moja kwa moja upade wa kusini ambapo Yanga walipanga koni na mipira kwa ajili ya mazoezi na kukutana na wachezaji wenzao kati.

Yanga waliingia uwanjani saa 10:15 mchezaji wa kwanza akiwa Max Nzengeli akifuatiwa na Abutwalib Mshery na Djigui Diarra ambao walielekea upande wa kusini mwa lango.

### NAPE AZINDUA WI-FI

Katika hatua nyingine, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, jana alizindua Wi-Fi ya bure uwanjani hapo ikiwa ni zawadi ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa wanamichezo waliojitokeza kushuhudia mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga kuanza rasmi kuitumia.

Wazi Nape, alisema kuwa ameagizwa na Rais Samia kuleta zawadi kwa wanamichezo wote waliojitokeza ndani ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa ni sehemu ya ukarabati wa dimba hilo.

"Ametuagiza tuhakikishe viwanja vyote vinakuwa na huduma hii na tumeanza na Uwanja wa Benjamin Mkapa na vingine vitafuata, leo tunaanza na mchezo huu wa watani wa jadi.

"Hiyo ni zawadi ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa wapenda michezo wote ili mfurahie mpira huku mkituma picha kumshukuru Rais Samia," alisema Nape.

Alisema watu wote walioko uwanjani wanaweza kuchati na kutuma picha wakiwa wanaendelea kufurahia burudani ya mpira.

"Ndugu zetu Azam Tv sasa wanaweza kurusha matangazo yao kwa kasi ya 4k ndio maana Rais Samia anasema kazi iendelee," alisema Nape.

### KIKOSI KILICHOANZA

**Simba:** Shomari Kapombe, Mohamed Hussein, Che Fondoh Malone, Henock Inonga, Fabrice Ngoma, Sadio Kanoute, Saido Ntibazonkiza, Jean Baleke, Clatous Chama na Kibu Denis.

**Yanga:** Djigui Diarra, Yao Kouassi, Joyce Lomalisa, Dickson Job, Ibrahim Bacca, Khalid Aucho, Mudathir Yahya, Maxi Nzengeli, Pacome Zouzoua, Stepane Aziz Ki na Kennedy Musonda.

# Michezo

Jumatatu Novemba 6, 2023

Nipashe



Madrid yakana kuteta na Mbappe UKURASA 22

# Yanga ipewe maua yake

Adam Fungamwango na

Saada Akida

## ●●● Yaichakaza Simba 5G, yarudia rekodi ya mwaka 1968, Nzengeli nusura amfikie Kibadeni lakini...




Wachezaji wa Yanga wakimkaba mfungaji wa bao pekee la Simba, Kibu Denis, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Chini ni mashabiki wa Yanga wakishangilia ushindi wa mabao 5-1 walioupata katika mchezo huo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



YANGA inastahili kupewa maua yake kwa kurejesha historia ya mechi ya dabi kufungana idadi kubwa ya mabao baada ya jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuifumua Simba 5-1 na kukwea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzanzania Bara ikifikisha jumla ya pointi 21 kwa michezo minane iliyocheza.

**Simba ilishindwa kuhimili vishindo vya Yanga kipindi cha pili na kukubali kufungwa mabao manne, baada ya timu hizo kwenda mapumziko zikiwa sare ya bao 1-1.**

Mabao yote ya Yanga yalifungwa na wachezaji wa kigeni, Mkongomani Maxi Nzengeli akipachika mawili nyavuni, Muivory Coast Pacome Zouzoua, Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki na Mzambia Kennedy Musonda.

Rekodi ya watani wa jadi, inaonesha kuwa mwaka 1968 Yanga iliichapa Simba mabao 5-1, mwaka 1977 Simba iliikung'uta Yanga mabao 6-0, rekodi ambayo hadi leo haijavunjwa na mwaka 2012 ambapo Simba iliiadhibu Yanga mabao 5-0, zote hizo zikiwa ni mechi za Ligi Kuu.

Mwaka 2020, Simba iliifunga Yanga mabao 4-1 kwenye mechi nusu fainali ya Kombe la FA, hivyo ushindi wa jana unaingia kwenye rekodi ya timu hizo kufungana mabao mengi kwenye mechi moja.

Nzengeli, aliyefunga mabao mawili kama angepewa penalti ya dakika ya 85, angeweza kupata mabao matatu 'hat-trick' na kuifikia rekodi ya mkongwe Abdallah Kibadeni, aliyefanya hivyo mwaka 1977, Simba ikichapa Yanga mabao 6-0.

Yanga iliandika bao la mapema dakika ya tatu tu ya mchezo likiwekwa wavuni na Mzambia, Kennedy Musonda, akiruka juu na kuunganisha kwa kichwa mpira wa krosi ya Yao Kouassi.

Bao hilo lilitokana na wachezaji wa Yanga kujenga shambulizi upande wa winga ya kulia na mpira ukaokolewa na mabeki wa Simba, lakini haukwenda mbali.

Ulinaswa na raia huyo wa Ivory Coast ambaye alisogea kidogo na kupiga krosi ya juu, mfungaji akiwa katikati ya mabeki wawili wa Simba, Henock Inonga na Che Malone Fondoh, ambapo aliruka juu na kuukwamisha wavuni.

Hata hivyo, bao hilo lilidumu kwa dakika sita tu, kwani dakika ya tisa Simba ilisawazisha kupitia kwa Kibu Denis. Mchezaji huyo naye alifungwa bao hilo kwa kichwa akiunganishwa mpira wa kona kutoka kwa Saido Ntibazonkiza.

Kona hiyo ilitokana na kipa Djigui Diarra kupangua mpira wa faulo uliopigwa na Clatous Chama baada ya Dickson Job kumchezea madhambi Saido nje kidogo ya eneo la hatari.

Kibu alipiga kichwa kwenye 'kona ya kwanza ya goli na mpira ukaenda kujaa kona ya pili, likiwa ni bao lake la kwanza msimu huu na la pili kwa Simba kufungwa kwa kichwa, la kwanza likiwa la Fabrice Ngoma dhidi ya Mtibwa Sugar, ikishinda 4-2.

Baada ya mabao hayo timu zote zilionekana kuupozesha mpira na muda mrefu ulichezwa katikati na mashambulizi yalikuwa ni ya hapa na pale, Yanga ikijaribu kuutumia upande wa kulia ambako ndiko walikopatia bao la kwanza.

Yanga ilikosa nafasi ya kuweka bao la pili dakika ya 35 baada ya Musonda kushindwa kuunganisha mpira wa krosi kutoka winga ya kushoto iliyopigwa na Nzengeli.

Shomari kapombe mara mbili, alishinda kupiga krosi zake vizuri dakika ya 40 na 43 ambazo zingeweza kuipatia Simba mabao kama zingekutana na wachezaji wenzake.

Kipindi cha pili kichokuwa na mafuriko ya mabao kilianza kuwa kibaya kwa Simba kuanzia dakika ya 60 baada ya kuumia kwa Kibu ambaye kwa kiasi kikubwa aliwasumbua mabeki wa Yanga na viungo wao wasiwe huru hivyo kuharibu mipango yao yote.

Kibu aliumizwa na kipa Diarra ambaye alitoka langoni kwenda kuokoa mpira na baada ya kutolewa nje, mabeki wa Yanga na viungo wao wakawa watulivu na kuanza kuleta purukushani nyingi langoni mwa Simba ambao kama kawaida yao wamekuwa wakicheza bila kuwa na kiungo mkabaji asili.

Dakika ya 63, Nzengeli alipachika mpira wavuni bao la pili kwa mguu wa kushoto baada ya kupata pasi kutoka kwa Stephane Aziz Ki kutokana na makosa ya walinzi wa Simba waliokuwa wakiwasindikiza wachezaji wao bila kuchukua hatua.

Aziz Ki, alifunga bao la tatu dakika ya 73, baada kazi kubwa iliyofanywa na Pacome aliupora mpira katikati ya uwanja na kuambaa nao kabla ya kumpa Lomalisa ambaye alimuwekea mfungaji aliyeupachika wavuni akiwa amezungukwa na lundo la walinzi wa Simba.

Kwa mara nyingine tena dakika tano baada ya bao la tatu, Nzengeli aliukwamisha mpira wavuni likiwa ni bao lake la pili

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >